## BONANZA



'Mwalimu na Samia' lafanyika mkoa wa Singida mwaka 2024. Likihudhuliwa na RC Dendego

## ELIMU



RC Mhe. Dendego ameagiza waalimu kuwekeza nguvu ya ziada ili kuongeza ufaulu wa wanafunzi

## UCHAGUZI



Viongozi wapya wapongezwa na Kuapishwa kuwa tayari kuwahudumi wananchi.

## TANZIA



Ulale Mahala Pema Jaji Kipenka. Viongozi wakubwa wahudhuria mazishi ya Jaji mstaafu.


JARIDA LA

# SINGIDARS

TOLEO LA MWEZI NOVEMBER - DECEMBER, 2024


# UTATUZI WA KERO SINGIDA

Uk.. 02

"Nimefika kutatua kero zenu wananchi wa mkoa wa Singida

RC Mhe. Halima Dendego



RC Mhe. Halima Dendego



Katibu Tawala Mkoa wa Singida
**Dkt. Fatuma Mganga**

### UCHUMI: IKUNDI 17 KUNUFAIKA MIKOPO



Vikundi 17 kunufaika Mikopo ya milioni 278.2 kwa asilimia 10 vikwahusisha Wanawake, Vijana na Walemavu

### WALIMU WA IRAMBA NA ADHA YA USAFILI



Walimu wakabidhiwa Pikipiki kupunguza adha ya Usafiri kazini. Mkuu wa Wilaya ya Iramba Mkoani Singida Suleiman Yusuph Mwenda akimkabidhi pikipiki Mwalimu Mkuu wa Shule

### MRADI YA UJENZI WA SHULE



Mradi wa boost waboresha shule ya msingi Unyamikumbi

### SULUHISHO LA KILIMO SINGIDA



Wakuu wa Idara za Kilimo Mkoani Singida wamepewa wiki mbili kuandikisha wakulima kwa asilimia 100.

### MAGARI MAPYA KWA RUWASA



Magari hayo yametolewa ikiwa ni jitihada za kuhakikisha kwamba mamlaka hiyo zinasaidia kutatua kero za maji katika Mkoa wa Singida.

### ELIMU: WAHITIMU VYUO VIKUU



'Fikirieni Kujiajiri baada ya kumaliza elimu zenu za vyuo vikuu' Mhe. Halima Dendego.
RC awaasa wahitimu vyuo vikuu kuacha kasumba ya kutegemea kuajiliwa pindi tu wanapomaliza elimu za juu nchini.

### KONGAMANO LA WASOMI NA UCHAGUZI



Mkuu wa mkoa ahudhulia kongamano la wasomi na maisha baada ya uchaguzi wa Serikali za Mitaa na Vijiji kwa wasomi katika Chuo cha Uhasibu kampasi ya Singida.

### SULUHISHO LA KILIMO SINGIDA



Wakuu wa Idara za Kilimo Mkoani Singida wamepewa muda wiki mbili kuhakikisha wanaandikisha wakulima katika daftari la kilimo.

# "NIMEFIKA KWA AJILI YA KUTATUA KERO ZENU" RC DENDEGO.



*Mkuu wa mkoa wa Singida Mhe. Halima Dendwgo akizungumza na wananchi katika ziara ndani ya wilaya ya Itigi kata ya Rungwa, Kalangali, Mwamagembe na Mitunduni mnamo tarehe 4 Disemba 2024.*

01 November 2024

Mkuu wa Mkoa wa Singida, Mhe. Halima Dendego amefanya ziara ya ukaguzi miradi na kusikiliza kero za wananchi katika Halmashauri ya Wilaya ya Itigi, Kata ya Rungwa, Kalangali, Mwamagembe na Mitundu iliyoanza siku ya Jumanne Novemba 4, 2024

Hayo yamejumuisha ukaguzi wa miradi mbali mbali ikiwemo ukaguzi wa zahanati mpya ya Itumba, ukaguzi wa nyumba za watumishi, kukagua mradi wa ujenzi wa Sekondari mpya ya Kalangali katika ziara hiyo.

Miongoni mwa kero zilizowasilishwa na wananchi ni uchache wa watumishi na vitendea kazi mashuleni na katika taasisi za afya, uhitaji wa umeme na maji, barabara, mahitaji ya mbolea na mbegu za ruzuku.Pia malipo ya wakati kwa watumishi na usikivu wa Redio katika maeneo hayo yenye usikivu hafifu yaliwasilishwa na wananchi ili kutatuliwa na Mkuu wa Mkoa.

Akizungumza na wananchi katika maeneo tofauti, Mkuu wa Mkoa Mhe. Halima Dendego ameahidi utatuzi wa kero hizo mbali mbali kwa wananchi ikiwemo kero ya umeme katika maeneo hayo na kuagiza utekelezaji wake ndani ya siku saba katika kata ya Rungwa katika eneo la Sekondari.

Pia,amewaagiza maafisa kilimo kuhakikisha wanatoa elimu kwa wananchi kuhusu suala la mbegu, pembejeo, dawa za kuua wadudu na mbolea za ruzuku ili kuwapa uelewa juu ya suala hilo na kuwashauri wananchi kujiandikisha katika daftari la pembejeo za kilimo ili kuweza kufaidika na huduma hizo zenye gharama nafuu kwa kusambazwa na mawakala na vyama vya msingi.

"Nitoe rai kwa wananchi kujiandikisha katika daftari la kilimo bure kabisa bila malipo ili kuweza kupata huduma ya mbegu, mbolea za ruzuku, viuatilifu pamoja na pembejeo kwa bei nafuu kabisa kwa maendeleo makubwa ya kilimo." alisema RC Dendego

Sambamba na hilo,Mkuu wa Mkoa ameagiza utekelezaji imara wa Shule ya Sekondari Mpya ya Kalangali iliyopo katika hatua za awali za ujenzi, huku akitoa muda kwa wahusika wa ujenzi wa nyumba ya mtumishi na zahanati ya Itumba kuhakikisha inakamilika katika viwango bora zaidi kuliko ilivyo sasa.

"Serikali imewekeza fedha nyingi katika kuhakikisha huduma bora zinawafikia wananchi hususani katika utoaji wa fedha za kutosha za ujenzi wa nyumba za watumishi na zahanati pia, hivyo ni jukumu letu kuhakikisha zinajengwa kwa ubora wa hali ya juu zinazosadifu gharama zinazotolewa" alisema Mhe. Dendego.

Charles Clement Mgama na Stephano Minja wananchi kutoka kata ya Rungwa ni miongoni mwa wananchi walifurahia ujio wa Mkuu wa Mkoa wa Singida katika wilaya ya Itigi wakisema wana imani kubwa kuwa changamoto zao zinakwenda kupatiwa ufumbuzi wa kero mbali mbali.

"Ujio wa Mkuu wa Mkoa utaleta ufumbuzi katika changamoto zetu nyingi ikiwepo changamoto ya umeme, maji, barabara, utatuzi wa migogoro ya ardhi, watumishi na nyinginezo kwani tunaamini zimefika kwa mtu sahihi ambaye ni daraja kati yetu na serikali kuu" alisema Mgama.

## TANZIA

Pumzika kwa amani Jaji Kipenka.



*Mkuu wa mkoa wa Singida Mhe. Halima Dendwgo,kushoto ni Naibu waziri wa aridhi, nyumba na maendeleo ya makazi Mhe.Joseph Pinda , kulia ni mkuu wa wilaya ya I Iramba Mhe. Suleiman Mwenda wakiwa katika hafla ya mazishi ya mwili wa Jaji mtaafu wa mahakama kuu Tanzania mnamo tarehe 6 Disemba 2024 katika wilaya ya Iramba mkoani Singida.*

06 November 2024

Mkuu wa Mkoa wa Singida Mhe.Halima Dendego ameshiriki mazishi ya marehemu Jaji Kipenka Msemembo Mussa, Jaji Mstaafu wa Mahakama Kuu ya Tanzania November 06, 2024 katika Kijiji cha Kinampanda kilichopo wilaya ya Iramba mkoani Singida.

Katika mazishi hayo aliungana na viongozi wengine akiwepo Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi Mhe. Geophrey Mizengo Pinda, Jaji Mkuu wa Tanzania Mhe. Prof. Ibrahim Hamis Juma, Mkuu wa Wilaya ya Iramba Mhe. Suleiman Mwenda, na Mkuu wa Wilaya ya Singida Mhe. Godwin Gondwe.

Mazishi hayo yametanguliwa na Ibada ya kuaga mwili wa marehemu iliyofanyika nyumbani kwa marehemu Kinampanda na kuongozwa na Askofu wa kanisa la KKKT Dayosisi ya Kati, Dkt. Cyprian Hilinti.

Marehemu Jaji Kipenka Msemembo Mussa alizaliwa Desemba 28, 1954 na amewahi kushika nyadhifa mbalimbali Serikalini enzi za uhai wake ikiwemo Katibu wa Bunge, aliugua kwa muda na kupata huduma katika hospitali mbalimbali kabla ya kufariki Novemba 04, 2024.

# Wanafunzi Wapewe Misingi Ya Stadi Za Maisha Kuwaandaa Wakihitimu" RC Dendego.

05 November 2024

Mkuu wa Mkoa wa Singida Mhe. Halima Dendego ameagiza waalimu kuwekeza nguvu ya ziada ili kuongeza ufaulu wa wanafunzi pamoja na msingi wa kuwawezesha kuendana na mazingira ya mtaani baada ya kuhitimu elimu yao ya Sekondari.

Ameyasema hayo (Novemba 5,2024)alipotembelea Shule ya Sekondari Mitundu na kukagua ukamilishaji wa vyumba viwili vya madarasa katika Halmashauri ya Wilaya ya Itigi.

Akizungumza katika kikao na waalimu wa Shule ya Sekondari Mitundu amesema ni vema waalimu kuongeza nguvu za ziada ili kupunguza ufaulu mbaya kwa wanafunzi kutokana na matokeo yasiyoridhisha ya shule hiyo, akisema ni vema kuzitambua changamoto za wanafunzi na namna ya kuzitatua kupitia semina,na kutiwa moyo na watu waliofanikiwa kama Viongozi ambao watawaona kama mfano kwao ili kuwapa motisha ya kusoma kwa bidii.

"Pamoja na kusoma darasani,wanafunzi wafundushwe stadi mbali mbali za maisha ikiwemo kilimo,usafi, kishiriki katika michezo na mchaka mchaka ili kuchangamsha akili,pia ni vema kupewa adhabu pale inapostahili kwani ni namna ya bora ya malezi bora kwa kuwaandaa kuwa na tabia njema" alisema Dendego.

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Sekondari Mitundu,amesema waalimu wa Shule hiyo wameazimia kutumia njia mbali mbali ya kuongeza ufaulu wa wanafunzi ikiwemo kuanza kuweka kambi shuleni kwa madarasa ya mitihani (kidato cha pili na kidato cha nne) kwa kufundishwa muda kwa muda mrefu ma uangalizi wa karibu,pia kwa kujisomea wenyewe alfajiri.

"Kuanzia sasa tumejiandaa kikamilifu kwa ajili ya oparesheni kabambe ya kutokomeza ufaulu wa daraja la nne na daraja ziro, kwa kutumia njia mbali mbali za kibunifu na kuwaweka wanafunzi wetu karibu, itakuwa rahisi kuzitambua changamoto zao kwa urahisi na kuwaweka katika mazingira salama kiakili kwa ustawi wa taaluma zao." alisema mwalimu.

Sambamba na hilo, Mkuu wa Mkoa alihudhurua katika Mkutano wa kusikiliza na kutatua kero mbali mbali za wananchi wa kijiji cha mitundu na kuagiza ufuatiliaji katika utendaji kazi mzuri wa masuala ya huduma za afya, kilimo, matumizi ya stakabadhi ghalani, umeme na maji ya uhakika.

Pia amesisitiza mikopo ya wajasiriamali kutolewa kwa vijana, wanawake na walemavu hususani maeneo ya kijijini kwa lengo la kuinua uchumi wa mtu mmoja mmoja, kaya na kijiji kwa ujumla. Kutokana na mikopo hiyo kuwafikia wanufaika hao vijijini itakuwa chachu ya maendeleo ya sekta nyingine ikiwemo bara bara, vituo vya afya, umeme na maji kwani mzunguko wa fedha utakua mzuri na kuchochea maendeleo.

"Ni wakati sasa wa wananchi wa kijijini kufikiwa na mikopo ya wajasiriamali kwa wingi kuliko mjini,hivyo ni wajibu wako muhusika kuhakikisha unawabainisha wahitaji wenye vigezo husika ili nao wanufaike na mikopo hiyo ambayo ni mtaji tosha kwao katika safari ya kujikwamua kiuchumi".alisema Mhe. Dendego.

Naye Diwani wa kata hiyo, Bw. Masanja Patrick ametoa shukrani za dhati kwa serikali kutokana na maendeleo makubwa yaliyotokana na utekelezaji wa shuhuli mbali mbali za maendeleo katika eneo hilo ikiwemo ujenzi wa vyumba vipya vya madarasa, upanuaji wa kituo cha afya na kukarabati bara bara zinazounganisha makao makuu ya kata na miradi mingine mipya ambayo bado haijakamilika kwa asilimia mia moja.

John Jackson, mkazi wa Kijiji cha Mitundu akizungumza baada ya Mkutano wa kijiji na Mkuu wa Mkoa amesema wamefurahishwa na ujio wa Mkuu wa Mkoa katika kijiji chao kwani itakua chanzo cha utekelezaji mzuri wa changamoto zote za wakazi wa eneo hilo kupatiwa ufumbuzi.

"Kupitia ziara hii ni wazi kuwa changamoto zetu zinakwenda kutatuliwa kwa kiasi kikubwa,nasi tunafurahi kuona kiongozi wetu ana utayari wa kuja hadi ngazi ya kijiji kwa ajili ya kusikiliza na kutatua changamoto zetu hivyo tuna imani kuwa kuanzia sasa miradi na huduma mbali mbali zitakwenda vizuri kwani ufuatiliaji wake upo katika mikono salama."alisema Bwana Jackson










# Magari Mapya Kurahisisha Utendaji kazi RUWASA, Mamlaka za Maji na Usafi wa Mazingira Singida



06 November 2024

Mkoa wa Singida umepokea magari matano yenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 795 kwa matumizi katika Mamlaka za Maji na Usafi wa Mazingira na Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) Mkoa wa Singida kwa ajili ya kusimamia shughuli za sekta ya maji.

Magari hayo yamekabidhiwa leo (Novemba 6, 2024) na Mkuu wa Mkoa wa Singida, Halima Dendego, ni kwa ajili ya Mamlaka za Maji na Usafi wa Mazingira katika Wilaya za Singida mjini,Manyoni na Kiomboi, RUWASA Mkoa wa Singida na RUWASA Wilaya ya Iramba.

Meneja wa RUWASA Mkoa wa Singida, Lucas Said, amesema magari hayo yametolewa ikiwa ni jitihada za kuhakikisha kwamba mamlaka hiyo zinasaidia kutatua kero za maji katika Mkoa wa Singida.

"Kama unavyofahamu tunaendelea kufanya kazi kuhakikisha kwamba tunafikia malengo ya kufikia asilimia 85 vijijini na mijini asilimia 95 ifikapo Disemba 2025,tunaendelea na jitihada ili kufikia malengo haya ambayo ni pamoja na kupata vitendea kazi ili viweze kusimamia miradi ipasavyo," amesema Said.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Singida (SUWASA),Sebastian Warioba, amesema baada ya kukabidhiwa magari hayo watahakikisha wanafikia malengo ya kufikisha maji kwa wananchi kama ambavyo imeainishwa kwenye ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM).

"Sisi watumishi wa sekta ya maji katika Mkoa wa Singida tunakuahidi tutaendelea kuchapa kazi kwa umoja,uadilifu na kujituma ili tuweze kufikia yale malengo ambayo yameainishwa kwenye ilani ya CCM,tunatoa shukrani kwa Rais Samia Suluhu Hassan na Waziri wa Maji, Jumaa Aweso kwa namna wanavyotujari na kutusimamia katika kuhakikisha tunamtua ndoo mama kichwani," amesema Warioba.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Singida, Dendego,amesema kiwango cha upatikanaji wa maji kwa sasa kimefikia asilimia 68.2 vijijini na asilimia 86 mjini hivyo bado hakijafikia kwenye malengo ya ilani ya CCM.

"Kupewa magari haya tumeongezewa mwendo,tumeongezewa kasi na ari kuhakikisha ile miradi yetu tunayotekeleza sasa iweze kutekelezwa kwa kasi kubwa ili kufikia malengo yaliyopo kwenye ilani ya CCM kabla ya muda uliopagwa," amesema.

Dendego amesema Mkoa wa Singida umejiwekea malengo ikifika Juni 2025 malengo ya kufikia asilimia 85 kupeleka maji vijijini na asilimia 95 mjini yatakuwa yamefikiwa.

Amesema serikali chini ya Wizara ya Maji imekuwa ikiendesha kampeni ya kumtua ndoo mama kichwani hivyo ili kufanikisha kampeni hiyo ni lazima kuwepo na vitendea kazi kama magari.

# "Singida ipo tayari kukabiliana na VVU na tatizo la Afya ya Akili" Dkt. Mganga



*Watumishi wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Singida wakiwa katika Ukumbi wa Mafunzo maalumu Kuhusu Udhibiti wa VVU, UKIMWI na Ugonjwa wa Afya ya Akili yaliyofanyika katika Ukumbi wa Ofisi za Mkuu wa Mkoa Singida.*

28 November 2024

Watumishi kutoka Ofisi ya Mkuu wa Mkoa WA Singida leo tarehe 28, Novemba 2024 wamepatiwa mafunzo maalum kuhusu udhibiti wa VVU, UKIMWI na ugonjwa wa Afya ya akili kwa Watumishi wa Umma mahali pa kazi yaliyo fanyika katika ukumbi wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa kuanzia saa tatu kamili asubuhi.

Akiwasilisha mada kuhusu VVU na UKIMWI,Dr. Said Mgeleka ambae ni Meneja wa Mradi kutoka USAID AFYA YANGU mkoa wa Singida, ametoa mada kuhusu hali ya Maambukizi wa VVU na UKIMWI kwa,uwiano wa wagonjwa kijiografia,umri, Jinsia na Hali ya Ndoa, katika Mkoa wa Singida.

Pia amefundisha kuhusu matumizi ya dawa kinga za VVU kabla na baada ya hatari ya Maambukizi (PEP na PrEP, aidha alitoa mada ya namna ya kujipima VVU kwa usiri Kwa mtu mmoja mmoja.

Kuhusu Maambukizi ya VVU kwa Jinsia Amesema kuwa takwimu zinaonyesha kuwa jinsia ya kiume imekuwa nyuma katika kupima VVU NA UKIMWI kwani kati ya jumla ya wateja 27,678 waliopo kwenye Huduma za Matibabu; wanaume ni ni 8,581 asilimia 31% pekee huku wanawake wakiwa 19,097

"Kundi linaloongoza Kwa maambukizi ya VVU na UKIMWI ni watu waliopo katika ndoa sababu kuu ikiwa ni kuwa na mpenzi zaidi ya mmoja huku kata ya Mandewa na Misuna ikitajwa kuongoza Kwa idadi ya maambukizi" amesema Dr.Mgeleka.

Naye Dkt.Lewis Rwegayula,ambaye ni Mratibu wa UKIMWI Mkoa wa Singidaa amewasilisha mada kuhusu tatizo la Ugonjwa wa Afya ya Akili akianisha sababu,dalili na matibabu ya afya ya akili huku akiwaasa watumishi kutumia muda vizuri kwa kuhakikisha wanamaliza majukumu yao Kwa wakati husika ili kuweza kuyamudu vema mazingira ya kazini na baada ya kazi,Pia kuyatambua mahitaji ya viongozi wao na kuyatekeleza vema ili kuepusha migogoro kazini itakayoweza kuwasababishia tatizo la afya ya akili kwa lengo la kuwa na matokeo mazuri katika kazi.

"Ni vema pia Kwa viongozi kuzitambua vema tabia za wasaidizi wao Ili kufahamu vyema namna gani watawaongoza na kuwasimamia katika utendaji wao wa kazi,pia Kila mmoja ayatambue mapungufu yake na kuyafanyia kazi ili kutokuwa sababu Kwa wengine kupata tatizo la afya ya akili".alisema Dkt Lewis

Pia amewasihi watumishi kuepuka kutumia dawa ambazo hawajaelekezwa na Daktari kwani nazo huchangia tatizo la Afya ya Akili.

Akizungumza Kwa niaba ya Kaimu Katibu Tawala Sehemu ya Afya,Ustawi wa Jamii na Lishe,Dkt.Shilla Mwashiuya amewaasa watumishi kuwashauri wenzao Wenye tatizo au dalili za afya ya akili ndani na nje ya ofisi Kwa kuwatia moyo wahusika na kuwasaidia pale inapowezekana na sio kuwavunja moyo na kuzidi kuwakatisha tamaa inayozidisha uwezekano wa kupata tatizo la Afya ya Akili.

Katibu Tawala WA Mkoa wa Singida,Daktari Fatuma Mganga akizungumza baada ya kuwasilishwa Kwa mada hizo amesema ni wakati sasa wa kuamua kunadilika kitqbia Kwa Kila mmoja kuhakikisha anajiepusha na mazingira yote yenye kuweza kusababisha maambukizi ya VVU huku akisisitiza watumishi kuwa na uthubutu wa kupima afya zao katika magonjwa ya kuambukiza na Yale yasiyoambukiza ili kuzifahamu Hali zao vema.

Kuhusu tatizo la Afya ya Akili amesema ni vema watumishi kutumia muda wao mwingi katika shuhuli za kujiingizia kipato baada ya kazi za ofisini ili kupunguza wimbi la watu Wenye tatizo la Afya ya Akili mara baada ya kustaafu akisisitiza matumizi Sahihi ya fedha na kutunza akiba Kwa manufaa Sahihi ya baadae.

"Tukapime afya zetu Kwa kupima magonjwa yanayoambukiza na yasiyoambukiza,Pia ni vema kufanya mazoezi ya viungo mara Kwa mara ili kuuweka mwili mbali na magonjwa"alisema Daktari Mganga.

## ZINGATIA

***Usijiwekee mipaka, Pima na jua Hali yako ili uwe na Maisha bora.***

***Elimu na Upendo vinajenga nguvu kubwa ya kukabiliana na VVU, na kutokomeza Unyanyapaa.***

# Kamati Ya Rufani Singida Wala Kiapo Cha Uadilifu



*Wajumbe wa kamati ya Rufani kutoka Wilaya tano za Mkoa wa Singida wakila kiapo cha utii na uadilifu, uaminifu na kutunza siri ili kuhakikisha haki kwa watu wote kwa mujibu wa sheria, katika uchaguzi wa Serikali za Mitaa na Vijiji.*

01 November 2024

Wajumbe wa kamati ya Rufani kutoka Wilaya tano za Mkoa wa Singida wamekula kiapo cha utii na uadilifu, uaminifu na kutunza siri kwa lengo la kuhakikisha haki kwa watu wote kwa mujibu wa sheria, katiba na kanuni katika uchaguzi wa serikali za mitaa.

Tukio hilo limefanyika Novemba Mosi, 2024 katika ukumbi wa ofisi ya Mkuu wa Singida likishuhudiwa na Hakimu Fadhili Enock Luvinga.

Akizungumza wakati wa tukio hilo, Katibu Tawala wa Mkoa wa Singida Daktari Fatuma Mganga amesisitiza mshikamano katika kamati za wajumbe wote kwa kufikia makubaliano mazuri yenye tija katika kushuhulikia taratibu zote za uchaguzi kwenda vizuri.

"Mkatumie nafasi zenu vizuri katika kusaidia mkoa wetu ili zoezi zima la uchaguzi liende vizuri na kuridhisha wagombea na wananchi kwa ujumla."alisema

Daktari Mganga amesisitiza wajumbe kupitia kanuni za uchaguzi wa serikali za mitaa kwa lengo la kupata au kuwa na uelewa wa kutosha juu ya kanuni za uchaguzi ili kutoa maamuzi bora yenye tija na kudumisha amani,upendo na mchakato bora wa uchaguzi mkoani Singida,Pia ameahidi kama Ofisi ya Mkuu wa Mkoa kutoa ushirikiano kwa kamati hiyo ya rufani wakati wowote utakapohotajika kwa nia ya kuhakikisha shughuli ya uchaguzi inakwenda vizuri.

Nasema Kazeni Mwanasheria kutoka Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Singida,akitoa ufafanuzi kuhusu kiapo,amesisitiza kila mmoja akiishi kiapo hicho katika utekelezaji wa majukumu yao ikiwa ni pamoja na kufanya kazi kwa uadilifu kwani endapo mtu akienda kinyume na kiapo atachukuliwa hatua za kisheria.

"Ikiwa Kiapo ni tamko analotoa mtu ili akubali jambo fulani ,pale Utakapokula kiapo hiki,uadilifu uwe mkubwa sana katikai kazi hii nyeti na kiapo huki kitatumiwa kama kielelezo katika kukuchukulia hatua za kisheria pale utakapokengeuka na kwenda knyume na kiapo hiki"

Sambamba na zoezi hilo,wajumbe wa kamati ya rufani wamekabidhiwa mihuri itakayotumika katika shughuli nzima ya uchaguzi wa serikali za mitaa na kusisitizwa kuitunza vema ili kuepusha matumizi mabaya kwa watu wasiohusika.

# Mhe. Dendego azindua zahanati na kuzungumza na wanufaika wa TASAF




*Mkuu wa Mkoa wa Singida Mhe. Halima Dendego akizindua Zahanati ya Kashangu, Iliyoanza kujengwa kwa nguvu za wananchi na mwishowe kuungwa mkono na serikali na kukamilika kwa asilimia mia moja.*

01 November 2024

Mkuu wa Mkoa wa Singida, Mhe Halima Dendego amewatembelea na kufanya mkutano na wanufaika wa mfuko wa kunusuru kaya masikini TASAF na kusikiliza kero na maoni mbali mbali waliyonayo katika Kata ya Itigi Mjini,ikiwa ni muendelezo wa ziara yake katika Halmashauri ya Wilaya ya Itigi.

Miongoni mwa malalamiko aliyopokea ni kuondolewa kwa idadi kubwa ya wazee katika unufaika wa TASAF walioomba serikali iwarudishe wapate huduma hiyo kwani ni ngumu kwa wao kuweza kumudu gharama za maisha na kujitegemea ili kujiingizia kipato kwani utendaji kazi wao umepungua sana na afya zao kutokua imara kutokana na umri kusogea.

Akijibu kero hiyo, Mkuu wa Mkoa ametoa maagizo kwa waratibu wa TASAF kuhakikisha wanafanyia kazi suala hilo kwa kuwarejesha wale wote wanaostahili katika mfuko huo na kuhakikisha malipo kwa wale ambao hawajapata fedha zao ndani ya muda wa miezi miwili kushughulikiwa kwa wakati.

Pia,alizindua mradi wa ujenzi wa zahanati ya Kashangu, Kata ya Idodyandole, zahanati Iliyoanza kujengwa kwa nguvu za wananchi na mwishowe kuungwa mkono na serikali na kukamilika kwa asilimia mia moja.

Awali akisoma taarifa ya mradi, Kaimu Mganga Mfawidhi wa Zahanati ya Kashangu, Twahil Amdan amesema kukamilika kwa mradi huo kutasaidia watu zaidi ya 3200 kutoka katika maeneo ya Kashangu na maeneo ya jirani kupata huduma za afya bila kusafiri umbali mrefu kufuata huduma hiyo.

Akizungumza na wananchi baada ya kuzindua mradi huo, Mkuu wa Mkoa amewaagiza wahudumu wa afya kuzingatia huduma bora kwa kuhakikisha wazee, wajawazito na watoto wachanga chini ya miaka mitano wanapatiwa huduma bila malipo.Pia ameomba kuongezwa kwa wakunga wenye uzoefu wa muda mrefu kazini ili kuboresha na kutoa huduma bora na ya uhakika zaidi hasa katika masuala ya uzazi.

Pia ameahidi kutatuliwa kwa changamoto za uhaba wa maji ya kutosha katika eneo hilo, umeme, nyumba za watumishi na vyoo vya wafanyakazi kama miongozo inavyoelekeza.

Kupitia mradi huo,wananchi wataepukana na adha ya kusafir umbal mrefu kufuata matibabu,kusaidia wakina mama wajawazito kupata huduma wakati wa ujauzito na kujifungua,kurahisisha upatikanaji wa huduma za uzazi wa mpango,chanjo na ufuatiliaji wa karibu wa makuzi ya watoto chini ya umri wa miaka mitano.Pia utapunguza idadi ya wakina mama wanaojifungulia nyumbani au kwenda zahanati wakiwa katika hatua za mwisho za kujifungua.

# Mfumo wa e-board kurahisisha shughuli za uaandaaji wa vikao.




Mfumo wa E- Board ni mfumo ambao umesanifiwa na kutengenezwa na Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) ili kutumika kuwezesha uratibu wa shughuli za uandaaji wa vikao mbalimbali vya bodi na menejimenti katika Halmashauri na Taasisi za Umma .


Mfumo wa e-board utarahisisha na kuwezesha uratibu wa shughuli zote za uandaaji wa vikao mbalimbali vya bodi na menejimenti katika Halmashauri na Taasisi za Umma.

Akizungumza kuhusu Suala hilo,Mkuu wa Kitengo Cha Teknolojia na Tehama Kutoka Ofisi ya Mkuu wa Mkoa,Bw.Baraka Mhembano amesema kuwa, mfumo wa e- board umebeba taswira ya shughuli zote zinazofanyika katika utaratibu wa kawaida wa uandaaji vikao kwa lengo la kuboresha uratibuji wa vikao vya bodi, menejimenti na halmashauri.

"Mfumo unalenga kuwasaidia wahusika kuandaa vikao yani sekretarieti katika kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi zaidi pamoja na kuwaongozea ufanisi wajumbe katika utekelezaji wa majukumu yao kupitia TEHAMA.Mfumo huu wa kidigitali utawezesha sekretarieti kuandaa yatokanayo kwenye kikao, wajumbe kupiga kura na kuwawezesha wajumbe wa menejimenti kutengeneza ripoti za utendaji kazi katika vipindi mbalimbali vya mwaka"

Mhembano alibainisha kuwa, mfumo wa e board umetengenezwa na kusanifiwa na wataalamu wa ndani kutoka e-GA na umekidhi uhitaji wa mchakato mzima wa uaandaji wa vikao kuanzia kwenye utengenezaji wa ajenda, utumaji wa notisi kwa wajumbe, utengenezaji wa makalablasha ya vikao, uchukuaji wa yatokanoyo, hadidu za rejea, upigaji kura pamoja na ripoti mbalimbali za utekelezaji.

Aliongezea kuwa, e-GA iliazimia kutengeneza mfumo wa eBoard ili kusaidia taasisi za umma kuwa na ufanisi kwenye eneo la kuratibu vikao baada ya kuona uhitaji mkubwa wa matumizi ya TEHAMA kwenye eneo hilo.



# Singida tujilinde na maambukizi mapya ya VVU na UKIMWI.



*Mkuu wa Wilaya ya Singidaa mkoani Singida akiwa katika siku ya maadhimisho ya Siku ya UKIMWI Duniani ndani ya Halmashauri ya Manispaa ya Singida ndani ya ukumbi wa Chuo cha Uhasibu Kampasi ya Singida.*

01 November 2024

Hayo yamesemwa na Mkuu wa Wilaya ya Singida Leo hii katika maadhimisho ya siku ya UKIMWI duniani Disemba Mosi, 2024 amemuwakilisha Mkuu wa Mkoa wa Singida Mhe.Halima Dendego yakiyoadhimishwa katika Halmashauri ya Manispaa ya Singida katika chuo Cha uhasibu kampasi ya Singida.

Akizungumza katika maadhimisho hayo,ametoa wito Kwa vijana kupima afya zao ili kuweza kuziishi ndoto zao nyingi huku akiwasisitiza wanandoa kuwa waaminifu ili kuepuka ongezeko la maambukizi huku akisisitiza tohara Kwa wanaume kama njia mojawapo ya kuzuia magonjwa Kwa wanaume

"Wanandoa wawe waaminifu Kwa wenza wao,pia ni vema kuwapenda,kuwajali na kuwahudumia waathirika WA VVU.Pia ni vema vijana wakaacha tamaa za maisha mazuri ili kuepuka vishawishi ambavyo vinasababisha kujiingizia katika vitendo vinavyoweza kupelekea kupata VVU, kuepuka hilo ni vema kuishi katika uhalisia WA maisha Yao na kupambania ndoto zao za baadae".amesema Gondwe.

Said Mgeleka ambaye ni Meneja wa Mradi kutoka USAID amesema kwasasa dawa za kufubaza virusi vya UKIMWI zinapatikana Kwa urahisi na Kwa wingi tofauti na miaka ya nyuma ambapo iliwalazimu watu wa makundi maalum pekee kama wamama wajawazito wakati WA kujifungia pekee na wagonjwa wale ambao CD4 zao zilianza kushuka na kusumbuliwa na magonjwa nyemelezi ndio waliokua wakipata dawa hizo kutokana na uchache wa dawa uliosababishwa na ufinyu WA bajeti

"Kwasasa dawa za ARV zinapatikana katika ngazi zote sio tu katika hospitali za mikoa na Taifa Bali mpaka katika zahanati zote vijijini kwani tangu 2016 juhudi za Serikali na wadau zimewezesha utoaji wa dawa hizo Kwa yeyote yule atakayegundulika na maambukizi bila Kujali wingi wa CD4 au dalili yeyote ya magonjwa nyemelezi"amesema Dkt.Mgeleka

Amesema pia kwasasa huduma za kinga dhidi ya VVU zimeongezwa Kwa kuleta dawa kinga Kwa watu wote walio katika hatari ya kuambukiza au kupata VVU,Pia kwasasa ni rahisi kupima wakati wowote na mahali popote na Kwa usiri kwani vifaa vya kujipima maambukizi vinapatikana kwa wingi na sio katika vituo vya afya pekee kama wakati wa nyuma.

Amini Nyaungo ni mmoja wa vijana ambao wamejitokeza katika maadhimisho haya amesema kuwaa ameitumia siku hii vema Kwa kupima afya yake pia kupata elimu juu ya VVU NA UKIMWI ambayo ataiwasilisha pia Kwa vijana wengine ambao hawana uthubutu katika kupima na kupata elimu ya VVU na UKIMWI.

"Nitaitumia fursa hii Kwa kuwapa vijana wenzangu elimu juu ya VVU, pia ntawaekimiaha kuhusu matumizi ya dawa kinga Kwa lengo la wao kufahamu Nini wafanye pale ambapo wanaona kuwa wapo katika hatari ya kupata VVU na matumizi Sahihi ya ARV Kwa wale ambao wamegundulika kuathirika na ugonjwa huu ila wana hofu ya kuanza kutumia dawa za kufubaza virusi"alisema Nyaungo.

Maadhimisho hayo yametanguliwa na maandamano mapema asubuhi, ikifuatiwa na huduma ya kupima afya (VVU NA UKIMWI) na mjadala kuhusu UKIMWI na vijana jinsi gani watajilinda na maambukizi au jinsi gani ya kuepuka kuambukiza wengine VVU.




# RC awakutanisha viongozi vyama vya siasa, wasisitiza amani.



*Baadhi ya Viongozi wa vyama vya Siasa mkoani Singida wakiwa kwenye kikao ndani ya Ofisi za Mkuu wa Mkoa wa Singida juu ya kuwepo na Kampeni za Amani, Upendo katika kipindi cha uchaguzi wa Serikali za mitaa na Vijiji.*

25 November 2024

Mkuu wa Mkoa wa Singida Mhe.Halima Dendego amefanya kikao na wajumbe wa vyama vyote vya siasa vilivyopo mkoani Singida Kwa lengo la kusisitiza umoja,amani na utulivu kuelekea siku ya uchaguzi Novemba 27, 2024 kilichofanyika katika Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Leo asubuhi kutoka vyama mbali mbali ikiwepo CHADEMA, CUF, DEMOKRASIA MAKINI, UMD, CCM, NLD, NRA, ACT-WAZALENDO, UDP na CHAUMA.

Akizungumza katika kikao hichi amewapongeza wajumbe wa vyama hivyo Kwa kufanya kampeni za amani katika siku zote husika bila uvunjifu wa amani huku akisisitiza kudumishwa Kwa amani iliyopo sasa mpaka tarehe ya uchaguzi itakapowadia na hata baada ya uchaguzi .

"Sisi sote ni ndugu,uchaguzi WA Tanzania ni wa Singida pia,na amani ya Tanzania ni ya Singida pia,sisi sote ni wamoja,tuweke utofauti qa vyama na dini pembeni,Serikali imekamilisha taratibu zote zimeshakamilika,hivyo tarehe 27 ninaomba amani iliyopo muiendeleze na watakaochaguliwa wote tuwaunge mkono."alisema RC Dendego.

Pia amewahakikishia amani na ulinzi na kutosha katika wakati wote wa kampeni na uchaguzi na hata baada ya uchaguzi na kuwakaribisha katika Ofisi muda wowote watakapokua na changamoto akisema kuwa ni vema kutumia upinzani vizuri kwa kujenga maendeleo na amani pamoja na msingi Bora WA uchaguzi Mkuu mwaka 2025.

"Tunashindana Kwenye sera na mipango,-Tutumie upinzani Kwa amani na sera na sio vurugu katika siku ya uchaguzi,Tuijenge amani mwaka huu Kwa msingi Bora WA uchaguzi WA mwaka 2025"alisema RC Dendego.

Naye Mwenyekiti WA Chama Cha ACT Wazalendo Mkoa wa Singida Hamis Labia, amefurahishwa na kukutana kwa viongozi na wajumbe wa vyama vingine vya upinzani akisema ni njia Bora ya kujenga ukaribu Wenye matokeo chanya ya urafiki na undugu mwema Kwa kuweza kujadili changamoto zao na kuzipatia jawabu Kwa pamoja.

Samweli G.Malo,Katibu WA CHADEMA Mkoa wa Singida amesisitiza uchaguzi WA haki na uwazi Wenye upinzani WA kiitikadi na kisera,akiomba ulinzi kuimarishwa katika kulinda kura zinazopigwa na kusisitiza uaminifu Kwa mawakala.Pia amesema kuwa CHADEMA imetoa wagombea 3,240 katika vijiji 217 kati ya vijiji 442.

Akizungumza katika kikao hicho,Mwenezi wa CCM Mkoa wa Singida amesema kuwa kwasasa mazingira ya uchaguzi yamekuwa ya amani kuliko kipindi Cha nyuma kwani amani imekuwa nguzo muhimu katika wakati wote hasa wakati WA kampeni kwani wagombea wamekuwa wakinadi sera zao Kwa amani na utulivu wa Hali ya juu sana hivyo kufanya zoezi la uchaguzi kuwa la amani na utulivu zaidi katika maeneo yote na wanategemea muitikio mkubwa wa wananchi tarehe ya kupiga kura tarehe 27 Novemba.

# FIKIRIENI Kujiajiri Baada Ya Kuhitimu"- RC Dendego



*Baadhi ya Magari yaliyotolewa na Mkuu wa Mkoa wa Singida Mhe. Halima Dendego kwenda kufanya kazi katika Mamlaka za Maji na Usafi wa Mazingira na Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini Mkoani Singida.*

22 November 2024

Mkuu wa Mkoa wa Singida Halima Dendego amewashauri wahitimu wa taasisi ya Uhasibu Tanzania kufikiri zaidi kujiajiri badala ya kutegemea ajira za serikali na sekta binafsi.

Mhe.Dendego amesema hayo katika mahafali ya 22 ya chuo cha Uhasibu Tanzania tawi la Singida. , na mahafali ya 13 ya Tawi la Singida, yaliyofanyika chuoni hapo kuanzia ngazi ya cheti hadi uzamili.

" Nawaomba mfikirie zaid kujiajiri kuliko kuajiriwa vipaji mnavyo kama nilivyoona wanafunzi wakibuni mbinu mbalimbali za biashara kwani licha ya ajira kutoa fursa nzuri lakini kujiajiri kunatoa nafasi ya kuwa mbunifu na uhuru wa kufikia malengo yaliyokusudiwa"alisema Mhe.Dendego.

Akiongelea kuhusu wahitimu 1477 waliohitimu katika fani mbalimbali amesema idadi hiyo ni kubwa na faraja kubwa kwa Mkoa wa Singida hivyo wakiitumia katika kutengeneza ajira kutaleta mabadiliko

Kuhusu baadhi ya wanachuo wanao onyesha ubunifu, Mkuu wa Mkoa amesema serikali ya mkoa itashirikiana nao kwa karibu ili kuhakikisha wanafikia malengo yao huku akiwataka kutumia mitandao ya kijamii kama jukwaa la kutangaza ubunifu, kukutana na wateja, na kueneza mawazo mapya Badala ya kupoteza muda mitandaoni kwa mambo yasiyokuwa na manufaa kwani mitandao hiyo inatoa fursa kubwa ya kujitangaza, kukuza biashara, na kufikia mafanikio makubwa.

Awali,Mhe. Dendego alianza kwa kuzindua program ya 'Masters' ambayo itapatikana katika kampasi ya Singida huku akipongeza juhudi zinazofanywa na Taasisi ya Uhasibu Nchini (TIA), katika kuboresha miundombinu na kusimamia maendeleo ya Tawi lake la Singida, ikiwa ni pamoja na ujenzi wa jengo jipya la utawala litakalokuwa na ghorofa tano na kugharimu zaidi ya Shilingi bilioni 13.5.

Ameeleza kuwa maboresho hayo yanaashiria ukuaji wa chuo hicho na yanaongeza fursa kwa vijana kujifunza maarifa na ujuzi zaidi unaoendana na mahitaji ya soko la ajira.

"Serikali itaendelea kushirikiana na wanafunzi na uongozi wa chuo hiki. Nawaomba sana mkitumie chuo hiki kujipatia maarifa zaidi kwa ajili ya kuitumikia jamii katika kila nyanja," alisema Dendego.

Kwa upande wake, Afisa Mtendaji Mkuu wa TIA, Profesa William Palangyo, alisema kuwa kuanzishwa kwa shahada ya uzamili katika Tawi la Singida ni hatua muhimu itakayochochea ongezeko la wanafunzi wanaotamani kujiunga na chuo hicho.

"Hadi sasa, tayari tumewasajili wanafunzi 66 kwa shahada ya uzamili, ambao wanaendelea kupata maarifa na ujuzi zaidi kwa manufaa yao binafsi na ya taifa kwa ujumla," alisema Profesa Palangyo.

Naye Mjumbe wa Bodi ya TIA, Renatus Msangira, aliyemwakilisha Mwenyekiti wa Bodi hiyo, aliwahimiza wananchi kutumia fursa ya uwepo wa chuo hicho kwa kuongeza maarifa ambayo yataboresha maisha yao.

Jumla ya wahitimu 1,477 walitunukiwa vyeti vyao katika ngazi mbalimbali za masomo, zikiwemo cheti na stashahada kwenye fani za mahusiano ya umma, uhasibu, uongozi wa rasilimali watu, usimamizi wa biashara, pamoja na ununuzi na ugavi.

# Mkurugenzi wa Singida awapongeza viongozi wapya wa serikali za mitaa


*Viongozi wapya wa Serikali za Mitaa na Vijiji wakila viapo baada ya kuchaguliwa kwa kura za ushindi na wananchi ndani ya kata zote. Viapo hivyo vinafanyika mbele ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Singida.*

28, November 2024

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Singida, Bi. Joanfaith Kataraia, amewapongeza viongozi wapya wa Serikali za Mitaa na kuwaasa kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi, ikiwa ni pamoja na kusimamia mapato, miradi ya maendeleo, na kuwa sauti ya wananchi kwa kusikiliza kero zao.

Kauli hiyo imetolewa leo, Novemba 28, 2024, wakati viongozi wapya wa Serikali za Mitaa kutoka Kata zote walioshinda kula kiapo katika Ukumbi wa Chuo cha Maendeleo (FDC), Manispaa ya Singida.

Viongozi hawa ni pamoja na wenyeviti wa mitaa, vijiji na vitongoji, pamoja na wajumbe mchanganyiko na wajumbe wanawake, ambao walipigiwa kura katika uchaguzi wa Serikali za Mitaa uliofanyika Novemba 27, 2024, kote nchini.

Bi. Kataraia aliwapongeza viongozi hao na kuwaasa kuzingatia majukumu yao muhimu katika utawala wa Serikali za Mitaa.

Alisisitiza kwamba viongozi hawa wanapaswa kuhakikisha mikutano ya kijamii inafanyika, kutekeleza miradi ya maendeleo, kusimamia mapato na matumizi, pamoja na kutatua migogoro mbalimbali, ikiwemo migogoro ya ardhi.

"Mtakuwa na jukumu kubwa la kuhakikisha miradi ya maendeleo inatekelezwa kwa ufanisi na mapato yanakusanywa na kutumika kwa manufaa ya wananchi. Lakini, ni muhimu kuhakikisha usalama na amani katika maeneo yenu, na kusimamia masuala ya afya, elimu, mazingira na usafi," alisema Bi. Kataraia.

Pia, aliwakumbusha viongozi hao kuwa uchaguzi umemalizika, na kwamba ni wakati wa kuwahudumia wananchi bila kujali tofauti za kisiasa, kidini, au kijamii. Alisisitiza umuhimu wa viongozi hao kuwa mfano bora kwa jamii, kwa kuhakikisha demokrasia inajengwa na wananchi wanaunganishwa katika maendeleo.

"Tunawategemea nyinyi kuwa viongozi wa mfano, kuhakikisha kwamba mnafanya kazi kwa bidii na kwa manufaa ya wananchi wote. Msiache kumsaidia Mh. Rais (Dkt Samia Suluhu Hassan) na kuwaunga mkono wananchi katika juhudi za maendeleo," alisisitiza Bi. Kataraia.

TUME HURU YA TAIFA YA UCHAGUZI
TANZANIA

*“Uchaguzi wa Serikali za Mitaa na Vijiji mwaka 2024 umefanyika kwa Amani, Upendo na Mshikamano mkoani Singida na Tanzania kwa ujumla”*

# RC Dendego Azindua jengo la mabweni chuoni Shamsiya.




*Mkuu wa Mkoa wa Singida Mhe. Halima Dendego akiwa kwenye hafla ya kuzindua na kufungua jengo jipya la mabweni ya wanafunzi wa Chuo cha Shamsiya Singida.*

14, November 2024

Mkuu wa Mkoa wa Singida,Mhe Halima Dendego ameshiriki katika hafla ya kuzindua na kufungua Jengo la Mabweni ya wanafunzi Chuo cha Shamsiya Singida katika Manispaa ya Singida,eneo la Karakana,Kata ya Misuna.

Akizungumza katika hafla hiyo,Mhe Dendego amesema ni jambo la furaha kuona suala la elimu linatekelezwa kwa vitendo na si maneno pekee katika Mkoa wa Singida,kwa lengo la kutoa elimu bora yenye lengo la kutunza maadili na kuienzi amani iliyopo.

Mhe.Dendego amesisitiza kuitunza amani iliyopo kwa kuhakikisha hakuna nafasi ya chuki wala faraka kati ya mtu mmoja mmoja jambo ambalo linaweza kuhatarisha umoja na mshikamano uliopo baina ya watu wote.

"Tuzidi kuienzi,kuitunza na kuikumbatia amani,tusidanganyike kwa adui atakaeingia katikati yetu na kutuletea faraka,bali safari ya leo iwe safari njema katika kuitunza amani ya Singida."amesema Mhe.Dendego.

Sambamba na hilo ametumia fursa hiyo kuwakaribisha wawekezaji katika Mkoa wa Singida,katika kuwekeza kwenye sekta mbali mbali ikiwemo kilimo,uvuvi,biashara na kadhalika .

Pia, ameahidi ushirikiano wa kutosha kwa taasisi za dini na kuwakaribisha ofisini wakati wowote watakapokua na changamoto,yupo tayari kuwasikiliza.




**Elimu ni Mwanga na Ufunguo wa Maisha**

## NUKUU ZA LEO

***"Mti Mmoja Unaoupanda leo, ni Maisha yako ya Kesho."***

...

***"Singida ni Utajiri wa Kilimo na Maliasili; Tuitunze."***

# Wakuu wa idara ya kilimo kikaangoni kwa kutowafikia Wakulima



14, November 2024

Wakuu wa Idara za Kilimo Mkoani Singida wamepewa muda wiki mbili kuhakikisha wanaandikisha wakulima katika daftari la kilimo kufikia asilimia 85 au zaidi Kwa lengo la kuhakikisha wakulima wanapata huduma ya mbegu na mbolea za ruzuku kuelekea Msimu mpya wa kilimo.

Hayo yamesemwa na Mkuu wa Mkoa wa Singida Mhe.Halima Dendego wakati wa kikao Cha mrejesho wa wadau sekta ya kilimo kutathimini uandikishaji wa wakulima ambapo halmashauri zote za Mkoani Singida ziliwasilisha utekelezaji wa uandikishaji huo umefikia hatua gani ili kurahisisha upatikanaji wa mbegu na mbolea kuelekea Msimu wa kilimo ulionza sasa.

Akizungumza katika kikao hicho,Mkuu wa Mkoa wa Singida Mhe.Halima Dendego amesisitiza utendaji WA kazi Kwa bidii Kwa vitendo zaidi kuliko mikakati ya maneno isiyo ya vitendo akiwataka kutoka mijini na kuwafuata wakulima maeneo Yao mpaka vijijini wanapoishi ili kuwa rahisi kuwapata na kuwapatia elimu ya kilimo wakati wa kuwasajili.

"Msirudi nyuma,rudini kazini mkawe sababu ya wakulima wetu kufanya vizuri kwasababu tunataka kuona kilimo chenye tija kufikia Disemba 31 iwe asilimia mia moja.Tujitume wenyewe na tusisubiri maelekezo kutoka Kwa viongozi wa juu Bali tuende mpaka vijijini walipo tuwafikie Kwa urahisi na tuwape elimu ya kilimo juu ya mbegu na mbolea za ruzuku."amesema RC Dendego

Mkuu wa Wilaya ya Mkalama,Mhe.Moses Machali akizungumza katika kikao hicho amesema ni wazi kuwa wanalo jukumu kubwa la kuhakikisha wakulima wanajisajili hivyo amewashauri wakurugenzi kuvutumia vizuri vyama vya ushirika na AMCOS kurahisisha ufikiwaji mzuri na wa uhakika k a mkulima kuhudumiwa huku akisisitiza matumizi ya mfumo WA uandikishaji kiteknolojia katika simu ili kuwafikia wakulima wengi Kwa wakati mfupi.

Naye Katibu Tawala Msaidizi sehemu ya Kilimo na uzalishaji Bw Starnslaus Choaji amemhakikishia Mkuu wa Mkoa kufanyia kazi Yale yote yaliyoazimiwa katika kikao hicho na kuwataka wakuu wa Idara ya kilimo kukutana na kutatua changamoto zote zitakazojitokeza na kuonekana kikwazo katika kufikia malengo yaliyowekwa.

Pia amesema kuwa ni vema kuwahisha mbegu Kwa wakulima kwani mvua zinatarajiwa kuwa chini ya kiwango mwaka huu na kuainisha mawakala mbali mbali ambao wapo tayari kufanya nao kazi Kwa bei rafiki Kwa wakulima kumudu gharama na upatikanaji wa haraka.

Akizungumza baada ya kikao,Bw.Eli Jackson Muna kutoka Wilaya ya Ikungi Kata ya Ntutu amesema wakulima wanategemea mbegu na mbolea za ruzuku kuwahishwa mapema katika maeneo Yao ili kuweza kuzipata na kupanda mapema Kutokana na Hali ya hewa iliyopo huku akiomba mzunguko wa kupata huduma hiyo kuwa mfupi Ili kumfikia mkulima Kwa haraka zaidi.

Katika Mkoa wa Singida mpaka sasa wakulima 108,506 sawa na asilimia 34 wameandikishwa kati ya malengo ya wakulima 316,684 yaliyowekwa huku upatikanaji wa mbegu za alizeti ukiwa Tani 105 kati ya Tani hitajika 1206 na mahindi yakihitajika Tani 316,684.Mbolea mahitaji ni Tani 15,834 huku ikitumika Tani 3,501



# Kongamano la TAHLISO la uchaguzi na maisha baada ya Chuo lafana.



*Mkuu wa Mkoa wa Singida Mhe. Halima Dendego akiwa kwenye picha ya pamoja baada ya kushiriki kwenye kongamano TAHILSO katika chuo cha Uhasibu Singida likihusu Wasomi na Maisha baada ya Uchaguzi*

14, November 2024

Mkuu wa Mkoa wa Singida,Mhe.Halima Dendego ameshiriki kongamano katika chuo cha Uhasibu kampasi ya Singida lenye jina la Kongamano la wasomi na Uchaguzi wa Serikali za Mitaa na Maisha baada ya chuo kwa wasomi wa elimu ya juu na vyuo vya Kati.

Akizungumza katika kongamano hilo,amewaasa wanafunzi hao kutumia vzur ujana wao kwa kesho iliyo bora kwa kuzingatia Uzalendo,heshima,utii,na utulivu na Mtandao wa watu wazuri wenye nidhamu nzuri ili kujiletea heshima katika jamii .

Pia amewasisitiza kujiandaa vizuri kwa kutumia elimu yao wanayopata vyuoni ili kuweza kujiajiri kwani kijana kujiajiri na kujipatia fedha kwa nguvu zake mwenyewe humletea heshima amani na uhuru katika maisha yake.

"Msichague kazi,ni vema kujiajiri ili kuongeza kipato,Tuchakarike vijana kuongeza kipato kwani Ubora na amani ya nchi yetu ni kutupa fursa ya kupata kipato.Ujana ni fedha,nidhamu na kujiamini.Muda wa kuishi vyuo ni mfupi sana hivo tuutumie vzur kuandaa maisha mazuri ya baadae baada ya chuo.

Licha ya hayo amewaasa kuepusha mahitaji makubwa yasiyo ya lazima kwa wanavyuo ili kuepusha gharama zisizo na msingi kwa wazazi wao wanaowagharamia,bali kutumia muda wao mwingi kujisomea kwa bidii na kuepuka mahusiano ya kimapenzi wawapo vyuoni yenye fadhaa mbali mbali ikiwemo kufeli mitihani,vifo kutokana na gomvi za wivu wa kimapenzi na magonjwa ya ngono ikiwemo VVU na UKIMWI.

Awali Amaniel Samweli,akizungumza kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji wa Manispaa ya Singida,ametoa elimu ya hamasa juu ya uchaguzi wa Serikali za Mitaa akisisitiza kuwa ni haki yao kushiriki kupiga kura na kuwahimiza kujitokeza kwa wingi siku ya uchaguzi .

Peter J.Peter rais wa wanafunzi katika chuo cha uhasibu kampasi ya Singida na Godfrey Mtilabu,Katibu Mkuu wa TAHLISO wamezungumza kwa niaba ya wanafunzi wote kuwa wapo tayari kushirikiana na serikali katika zoezi zima la uchaguzi kwa kuhakikisha wanatoa taarifa yeyote yenye viashiria vya kuvunja amani katika sehemu husika kwa lengo la kutimiza wajibu na haki yao ya kidemokrasia.

"Tutaendelea kuwa waadilifu na wazalendo kwa Taifa letu,vijana hatutakengeuka na kupotoka bali tutakua pamoja daima kudumisha umoja na amani ya nchi yetu."amesema Godfrey.

Sambamba na hilo,wanafunzi wamepata elimu ya afya kutoka Shirika la Mega We Care juu ya ugonjwa wa UKIMWI,afya ya uzazi na matumizi sahihi ya dawa,Pia Mkuu wa Mkoa ameahidi kuanzishwa kwa ligi ya vyuo Mkoani Singida.

# KIPINDUPINDU Chatafutiwa Suluhu yake Singida.



*Katibu Tawala wa Mkoa wa Singida Dr. Fatuma Mganga akiwa kwenye kikao na Mganga mkuu wa Mkoa Dr. Victoria Ludovic na wadau mbalimbali ili kutokomeza ugonjwa wa kipindupindu mkoani Singida.*

22, November 2024

Katibu Tawala wa Mkoa wa Singida ameagiza uwajibikaji kwa timu ya uratibu wa afya Mkoa kuhakikisha wanajituma na kufanya kazi kwa weledi ili kuepusha mlipuko wa ugonjwa wa kipindu pindu katika Mkoa wa Singida.

Ameyasema hayo katika kikao kazi cha kujadili namna ya kukabiliana na ugonjwa wa kipindu pindu leo Novemba 22, 2024 kilichofanyika katika ukumbi wa Mkuu wa Mkoa wa Singida kikiratibiwa na mganga Mkuu wa Mkoa Daktari. Victorina Ludovick.

Akizungumza katika kikao hicho, Katibu Tawala wa Mkoa wa Singida, Daktari Fatuma Mganga ametoa maelekezo mbali mbali kwa timu ya uratibu wa afya Mkoa katika kukabiliana na ugonjwa wa kipindu pindu ikiwemo kutibu maji yote yanayotumika vijijini na visima vya watu binafsi majumbani,kuhakikisha kila kaya ina choo cha kutumia,timu kuweka kambi yenye vifaa vya kutosha katika maeneo hatarishi na kuhakikisha shule zote za Msingi na Sekondari Zina vyoo na sehemu za kunawia mikono pamoja na TARURA kuhakikisha wanarekebisha bara bara zote zisizo rafiki kurahisisha ufikiwaji rahisi wa maeneo yenye viashiria vya hatari.

"Kila mmoja wetu hapa ahakikishe anawajibika ipasavyo katika kuunga mkono juhudi za kupambana na kipindu pindu,wadau wote kila mmoja atumie nafasi yake kwa matokeo mazuri ya mpangokazi na kuleta mrejesho wa utekelezaji wa majukumu yake"alisema Daktari Mganga.

Pia amewaagiza kupima sampuli za maji katika maeneo tofauti tofauti ili kubaini visima vyenye vimelea vya ugonjwa wa kipindu pindu ili kuwa rahisi kuyatibu na kuepusha matumizi yake kwa wananchi wa maeneo husika.

Daktari Mganga ameagiza Uwajibikaji wa CHMT zote na RHMT na kutoa maagizo kwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Ikungi ikiwa ni pamoja kupeleka maafisa afya katika maeneo hayo muda wote kufuatilia na kuhakikisha kuwa kaya zote zina vyoo, vifaa vya kunawia mikono kila kaya, mashuleni, Maeneo yote ya biashara, Minada na mikusanyiko ili kumaliza Kipindupindu kabisa huku akitoa siku 14 kwa RHMT , RUWASA, DED IKUNGI kushirikiana na wadau ili kumaliza Kipindupindu haraka iwezekanavyo

Awali akiwasilisha taarifa juu ya ugonjwa wa kipindupindu,Afisa Afya wa Mkoa wa Singida Bw.Sebastian Mgeta,ameainisha visababishi mbali mbali vya ugonjwa huo ikiwemo ukosefu wa maji safi na salama katika maeneo yenye mlipuko,ukosefu wa vyoo katika kaya,baadhi ya kaya kutotumia dawa za kutibu maji,imani potofu na kuchelewa kwenda kupata matibabu pindi tu dalili zinapoonekana.

"Licha ya hayo changamoto za miundombinu ya barabara kutokua rafiki kunachangia kutofikiwa kwa urahisi kwa maeneo yenye viashiria vya ugonjwa huo,usibuaji kutofanyika kikamilifu,wagonjwa kuficha taarifa za ugonjwa na ushiriki hafifu wa baadhi ya viongozi unarudisha nyuma juhudi za kupambana na ugonjwa wa kipindu pindu.alisema Bw.Sebastian.

Pia ameainisha kazi mbali mbali zilizotumika kama njia ya kupambana na ugonjwa huo ikiwemo huduma ya usibuaji katika kaya mbalimbali mgonjwa anapobainika,kuhamasisha jamii kuhusu utumiaji wa vyoo bora na kutoa elimu maeneo mbali mbali,kutibu visima pamoja na vikao vyavujirani mwema kati ya Ikungi,Igunga na Uyuwi.

Akizungumza kuhusu changamoto ya maji katika maeneo yenye mlipuko,Meneja wa RUWASA Mkoani Singida Bw.Lucas Said amesema kuwa shirika lipo katika mikakati ya kutekeleza mradi wa ujenzi wa visima vya maji maeneo kadhaa kwa lengo la kuhakikisha wananchi wanapata huduma ya mahi safi na yaliyotibiwa.

Katika kikao hicho wajumbe wameazimia kushirikiana kwa pamoja kuepusha mlipuko zaidi wa ugonjwa wa Kipindu pindu huku wakiahidi kuchangia mahitaji mbali mbali yanayohitajika ili kuongeza kasi ya mapambano dhidi ya ugonjwa huo hatari.





# Bonanza la "MWALIMU NA SAMIA"lafanyika Singida.




*Walimu na wadau mbalimbali wa elimu wakiwa katika shamrashamra za Bonanza la 'MWALIMU NA SAMIA' lilofanyika kwa kushirikisha walimu kutoka Halmashauri za Mkoa wa Singida huku mgeni rasmi akiwa Mkuu wa Mkoa RC Dendego.*

06 November 2024

Mkoa wa Singida umeendaa Bonanza lililowaoutanisha waalimu kutoka Halmashauri mbili za Mkoa wa Singida,Halmashauri ya Manispaa ya Singida na Halmashauri ya Singida lenye Jina la "Bonanza la Mwalimu na Samia"lililofanyika katika uwanja WA Bombadia mkoani Singida likiratibiwa na Mkuu wa Mkoa na Mkuu wa Wilaya ya Singida.

Katika Bonanza hilo Mgeni rasmi akiwa ni Mkuu wa Mkoa wa Singida,ametoa pongezi Kwa waalimu hao kama daraja imara kati yao na wanafunzi katika nyanja za masomo Kwa kuwajengea uwezo imara na kuhakikisha wanafunzi hao wanapata ufaulu mzuri unaowawezesha kuendelea na masomo ya Sekondari na vyuo vikuu pamoja na msingi imara wa kujiajiri hata baada ya kumaliza masomo yao.

Amesema kuwa serikali inautambua mchango mkubwa WA waalimu na hivyo serikali itakuwa tayari wakati wote kuhakikisha wanasikiliza na kutatua kero zao ili kuendelea kuzitafutia ufumbuzi ili kuendelea kuwaunga mkono Kwa kuweka mazingira mazuri ya kufanyia kazi Kwa kujenga miundombinu Bora kuanzia shule ya awali na Sekondari na kuongeza vitendea kazi vya kutosha mashuleni.

"Waalimu wa Mkoa wa Singida mmeendelea kuwa baraka katika Mkoa huu kwani takwimu za ufaulu katika Mkoa wa Singida zinazidi kupanda juu tofauti na ilivyokua katika siku za nyuma kwani mnafanya kazi zenu Kwa weledi na uzalendo pamoja na changamoto zilizopo ambazo zitafanyiwa kazi"alisema Mhe.Dendego

Mkuu wa Wilaya ya Singida,Mhe.Godwin Gondwe akizungumza katika Bonanza hilo,amesema tuzo mbalimbali zinazotolewa Kwa waalimu ni kama motisha na zitasaidia kuongeza morali katika ufundishaji na kuwapongeza Kwa matokeo mazuri ikiwemo ya kidato Cha nne mwaka huu yaliyopanda ufaulu Kwa asilimia huku kukiwa na malengo ya kufuta daraja sifuri Kwa mwaka ujao wa 2025.

"Mpango wetu ni kuondoa daraja ziro kabisa mashuleni,hili litafanyika pia Kwa kuhakikisha wanafunzi wanapata vyakula mashuleni wote Kwa ujumla na sio Kwa madarasa ya mitihani pekee."alisema DC Gondwe

Naye mstahiki Meya wa Manispaa ya Singida,Yagi Kiaratu amesema serikali inaendelea kuunga mkono elimu Kwa kuhakiisha Kuna miundombinu Bora ya elimu kama kujenga mashule,madarasa ya kutosha,nyumba za waalimu,mabweni kufuta ada za wanafunzi kuanzia awali mpaka kidato Cha sita na kuongeza mikopo ya elimu ya juu ili kuwawezesha wanafunzi katika gharama za ada na kujikimu,Hivyo ni vema kuutambua mchango wa mwalimu kwa mkono mwalimu kwani ndie daraja la kuwezesha mafanikio ya wanafunzi.

"Ufaulu katika matokeo umeongezeka Kwa takribani asilimia Tano,hii ni kutokana na uboreshwaji WA mazingira ya kujifunzia na kufundishia Kwa waalimu na wanafunzi,ndio sababu ya mwitikio na hamasa kubwa inayoonekana Kwa waalimu kujitokeza Kwa wingi SIKU ya Leo kwasababu wana furaha kwani changamoto zao zinafanyiwa kazi.amesema Mstahiki Meya.

# Changamoto za Stakabadhi Ghalani kutafutiwa majawabu, Wakulima kunufaika zaidi.

10, November 2024

Mkuu wa Mkoa wa Singida, Mhe. Halima Dendego, amewatoa hofu wakulima wa dengu katika Halmashauri ya Wilaya ya Itigi kwamba tani 257,933 ambazo bado hazijauzwa kwamba zitauzwa na watalipwa fedha zao.

Akizungumza hayo leo Novemba 10,2024 baada ya kutembelea ghala la kuhifadhia dengu lililopo Itigi mjini, amesema serikali itahakikisha dengu iliyopo inauzwa na kwamba kwa Halmashauri ya Wilaya ya Itigi hadi sasa zimeuzwa zaidi ya tani 15 000.

"Dengu yetu kutoka Mkoa wa Singida tunauza nchini India,bahati nzuri hadi sasa sijapata malalamiko yeyote ya kwamba labda dengu yetu haina ubora hili jambo la kujivunia,"amesema.

Dendego amesema changamoto ambazo zimepatikana wakati wa utekelezaji wa ununuzi wa dengu kwa kutumia mfumo wa Stakabadhi Ghalani zitaendelea kutatuliwa na kwamba hivi karibuni kutaitishwa kikao cha wadau kujadili namna ya kukabiliana na changamoto hizo.

"Zipo changamoto za ukosefu wa maghala,vyama vya ushirika kufa,mizani na AMCOS kupitia kikao ambacho wadau ambacho tutakifanya changamoto hizi tutazojadili na kuona namna ya kuzipatia ufumbuzi,"alisema.

Awali Afisa Kilimo Halmashauri ya Wilaya ya Itigi, Mlagazi Mgalula, amesema zao la dengu limekuwa la kwanza kwa kuingiza mapato kwenye halmashauri ambapo tangu ununuzi ulipoanza Agosti Mosi, 2024 kwa kutumia mfumo wa stakabadhi ghalani wakulima wameweza kulipwa zaidi ya Sh.bilioni 19.

Amesema hivi sasa kuna changamoto ya upatikanaji wa wanunuzi katika dengu iliyopo kwenye ghala na kwamba halmashauri imefanya mipango kutafuta wanunuzi wengine badala ya kutegemea kuuza India tu.

Katibu wa AMCOS ya Mlowa, Emmanuel Daniel, amesema hivi sasa kuna wiki tatu bado minada haijafanyika hali ambayo imezua hofu kwa wakulima hasa ikizingatia kipindi hiki ni cha kuelekea msimu wa kilimo.

Daniel ameiomba serikali kufanya haraka kutafuta wanunuzi katika dengu iliyopo kwenye ghala ili wakulima waweze kulipwa fedha zao na hivyo wapate nguvu kuandaa mashamba yao.

Issa Adam Issa,mkulima anayefaidika na mfumo wa stakabadhi ghalani,ameonyesha kufurahishwa na mfumo huo amesema umekuja kuwanufaisha wakulima na kuhakikisha wanauza mazao yao kwa bei nzuri,ametoa wito kwa serikali kuhakikisha wanaboresha zaidi huduma hiyo ili watu wengi zaidi waweze kujiunga kwa kutumia njia mbalimbali kuwaelimisha hasa kwa kutoa elimu zaidi juu ya mfumo wa stakabadhi ghalani.





# "Halmashauri zibuni vyanzo vya Kudumu vya Mapato" DC Apson

31, November 2024

Katika mwaka wa fedha 2024/2025,halmashauri ya Wilaya ya Ikungi ilipanga kukusanya na kutumia jumla ya shilingi Bilioni 10.9 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kutoka kerikali kuu, huku wahisani na mapato ya ndani ikiwa ni bilioni 1.2 na mpaka sasa halmashauri imepokea jumla ya Shilingi bilioni 5 ambazo zinaendelea kutumika katika utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo wilayani hapa.

Akisoma taarifa katika baraza la madiwani Wilaya ya Ikungi tarehe 31 Octoba, 2024 ukumbi wa mikutano Halmashari, Mkurugenzi mtendaji Ndg Justice L. Kijazi amesema kuwa katika mwaka wa fedha 2024/2025 halmashauri ya Wilaya ya Ikungi katika bajeti yake ya utekelezaji wa miradi kwa fedha za mapato ya ndani hadi kufikia siku ya kikao hiki imepeleka jumla ya shilingi milioni 440 kutekeleza miradi kama vile Ujenzi wa nyumba 1 ya mwalimu katika shule ya msingi Magungumka, Ujenzi wa Matundu 32 ya vyoo na vyumba 6 vya madarasa katika shule za msingi za Nali, shule shikizi Sanya-Lighwa, Ufana, Mankumbi, Msosa, Shule shikizi Mtakuja-mwaru, Utengenezaji wa madawati ya wanafunzi kwa shule za msingi, Ukamilishaji wa miundombinu ya afya katika zahanati ya Muhintiri, Mwaru, tupendane, mgungira, Choda, Makhonda na vituo vya afya vya Irisya, Iyumbu na ntuntu, pamoja na Ujenzi wa matundu ya vyoo 29 katika shule za sekondari za Ighombwe, Masinda day, Ntuntu, Mang'onyi shanta, Miandi na Muhintiri.

Kwa upande wake Mkuu wa Wilaya ya Ikungi Mhe.Thomas Apson katika hotuba yake amesema kuwa kuna haja ya halmashauri kubuni vyanzo vya mapato vya kudumu kama vile kuanzisha vituo vya mafuta, vivutio ya kitalii, kuhifadhi misitu ili kuzalisha hewa ya ukaa pamoja na kuanzisha hoteli za kisasa vyanzo ambavyo ni vyakudumu tofauti na baadhi ya vilivyopo ambavyo vinaingiza mapato kwa msimu.

Naye mwenyekiti wa Halmashauri ya wilaya ya Ikungi Mhe.Ally J. Mwanga amewataka madiwani kuwa mabalozi wazuri katika ukusanyaji wa mapato wakishirikiana na watendaji wa kata na vijiji pamoja na utunzaji wa misitu kama vile msitu wa Mlilii pamoja na Msitu wa Minyughe kwa maslahi mapana ya Halmashauri yetu.



# Wazazi na walezi watakiwa kuhakikisha watoto wanapata Chanjo.



*Huduma ya chanjo kwa watoto ikitolewa kwa watoto mkoani Singida katika vituo vya afya na hospitali*

17 December, 2024

Wazazi Wilaya ya Iramba Mkoani Singida wametakiwa kuhakikisha wanawapeleka Watoto wao kwenye Vituo vya kutolea huduma za Afya kwa wakati ili wapate chanjo dhidi ya magonjwa yanayozuilika kwa chanjo.

Wito huo umetolewa Disemba 17, 2024 na Afisa Tarafa, Tarafa ya Kisiriri Bw. Oswald Leopord kwa niaba ya Mkuu wa Wilaya ya Iramba Mkoani Singida Suleiman Yusuph Mwenda wakati akizungumza katika uzinduzi wa Wiki ya Chanjo uliofanyika kwenye Zahanati ya Bomani.

Aidha Oswald ametoa rai kwa wazazi pamoja na walezi kuhakikisha watoto walio chini yao wamepata chanjo zinazotakiwa kwa wakati ili kuwakinga dhidi ya magonjwa hatari na kuachana na Imani potofu kuhusu chanjo.

"Nitoe rai kwa wazazi wote kuhakikisha watoto wote wanapata chanjo zinazotakiwa kwa wakati kama tunavyoelekezwa na wataalamu ili kuwakinga watoto dhidi ya magonjwa hayo hatari kama vile Surua na Polio.... zamani watu walikuwa wakipata matatizo kwa sababu ya kutochanja kwa sababu ya Imani potofu. Tuachane na imani potofu tuwapeleke watoto wapate chanjo." Alisema Oswald Leopord.

Kwa upande wake kaimu Mganga mkuu Halmashauri ya Wilaya ya Iramba Daniel Paul Nkingo amesema Lengo la uwepo wa wiki ya chanjo na mwezi wa matone ya Vitamini A ni kuendelea kukumbushana na kuhamasishana kuhusu umuhimu wa chanjo katika jamii, kuwa fatilia na kuwaibua watoto walioasi chanjo na ambao hawakupata chanjo tangu kuzaliwa kwa sababu zozote zile ili waweze kupata chanjo na kuwaepusha na magonjwa yote yanayozuilika kwa chanjo, kuwapatia matone ya nyongeza ya Vitamini A pamoja na upimaji wa hali za Lishe kwa watoto wenye umri wa miezi 6-59.

"Lengo ni kuwakinga dhidi ya magonjwa ya mlipuko yanayoweza kuzuiliwa na chanjo. Na tunaendelea kutoa Elimu na kuwaibua ambao hawajapata chanjo na walioasi chanjo ili wapate chanjo, kwa kufanya hivyo tunaamini Jamii yetu itakuwa imekingwa." Alisema Daniel Nkingo

Naye Mratibu wa chanjo Wilaya ya Iramba Jackson Shango Shillah amesema kuanzia January 2023 Hadi Novemba 2024 jumla ya watoto 1918 wameasi chanjo na zoezi hili litahusisha kuhakikisha wamepata chanjo.

# Mafunzo ya BOOST kwa Walimu wa Shule za Msingi



*Walimuu wa shule za Msingi Wilayani Iramba wapewa Mafunzo ya siku tatu kuhusu Matumizi ya njia na vifaa vilivyo boreshwa kufundishia na kujifunzia Mtaala wa Elimu ya awali kupitia Mradi wa BOOST.*

19 December, 2024

Akizungumza Disemba 19, 2024 katika ufunguzi wa mafunzo hayo kwa niaba ya Mkurugenzi wa Halmashauri Afisa Elimu Wilaya, Idara ya Elimu ya Awali na Msingi Halmashauri ya Wilaya ya Iramba Mwalimu Rose Willgeofrey Kibakaya amewataka Walimu Kuzingatia mafunzo hayo ili kuinua taaluma na kuwawezesha wanafunzi wa awali kufahamu kusoma, kuhesabu na kuandika.

"Nia ya Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan ni kubadilika tutoke hapa tulipo, Kwahiyo tuna Imani mtafundishwa vizuri na mtakuwa ni chachu kwa maendeleo ya Elimu Wilaya ya Iramba.Tunawategemea sana naomba mafunzo hayo myasikilize vizuri." Alisema Mwalimu Rose Kibakaya.

Kwa upande wake Afisa Tawala kutoka Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) idara ya Usimamizi wa Elimu Joyce Henry kitundu amesema zoezi hili ni kwaajili ya kuwawezesha Walimu wa awali kufahamu mitaala iliyoboreshwa ili kuitumia vyema katika ufundishaji.

"Tunataka Madara ya Elimu ya awali yaongee ili mtu alifika shule akutane na darasa lenye picha na vitendea kazi ili apende na kuhamasika kwenda kujifunza. Kwahiyo zile zana watakazozitengeneza Walimu zitawasaidia watoto namna ya kujifunza Elimu yao ya awali kabla ya Elimu ya Msingi." Alisema Joyce Henry

Mafunzo hayo yalianza Disemba 16-18, 2024 kwa Walimu Mahiri pamoja na mthibiti Ubora wa shule kwa ngazi ya Wilaya, na kuendelea kwa siku nne kwa Walimu wa awali na siku tatu kwa Walimu wakuu na na walimu wanaofundisha darasa la Awali yatahitimishwa Jumamosi Disemba 22, 2024.

# Wanaume Nguzo Muhimu Kuimarisha Huduma Za Afya Katika Jamii



*Picha ya pamoja na Timu ya Usimamizi na Uendeshaji wa Huduma za Afya mkoa na Wilaya, nje ya ukumbi wa Halmashauri ya Wilaya yaIkungi kwenye arsha ya Kuimarisha Huduma za Afya kwa kuwashirikisha Wanaume katika jamii.*

12 December, 2024

Timu ya usimamizi na uendeshaji wa huduma za afya mkoa na wilaya imeazimia kuhakikisha huduma za afya zinawafikia wanajamii wote kwa usawa, ikiwa ni pamoja na kushirikisha wanaume kikamilifu ili kuboresha afya zao wenyewe, afya za wanawake, watoto, na vijana.

Hayo yamesemwa leo, tarehe 12 Disemba 2024, katika ukumbi wa Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi kwenye warsha yenye lengo la kuimarisha huduma za afya kwa kushirikisha wanaume katika huduma za afya ya uzazi, mama, na watoto.

Bi. Desteria Nanyanga, mwakilishi kutoka Wizara ya Afya akitoa mafunzo, amesema kuwa warsha hii ni muhimu kwani wanaume ndio watoa maamuzi katika familia, na hii itasaidia kuvunja vikwazo vya kitamaduni, kuboresha huduma za afya ya uzazi kwa vijana, kupunguza ukatili wa kijinsia, na kuhakikisha kuwa wanawake na watoto wanapata msaada muhimu wakati wa ujauzito, kujifungua, na baada ya kujifungua.

Kwa upande wake, Kaimu Mganga Mkuu wa Mkoa wa Singida, Bi. Teda David Sinde, akifungua warsha hiyo, amesema matarajio yake mara baada ya warsha ni uelewa wa pamoja kuhusu ushiriki wa wanaume katika afya ya uzazi, mama na mtoto, na kuboresha huduma za afya katika wilaya ya Ikungi. Alisisitiza kutumia vyema uzoefu wa washiriki kutoa maoni ili mpango huu uweze kufanikiwa.

"Tunakusudia kuwasilisha na kukusanya maoni na mapendekezo ili kuboresha mwongozo huu na kuhakikisha unafaa kwa utekelezaji ngazi ya mkoa, halmashauri, na jamii kwa ujumla," alisema Sinde.

Kwa upande wake, Bi. Nkinda Shekalagwe, mwakilishi kutoka Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), aliwaomba wote waliopata elimu hiyo kwenda kuwa walimu wazuri kwa wenzao ili kuhakikisha huduma za afya wilayani Ikungi zinakuwa bora, husussan upande wa afya ya uzazi na lishe.

Wakitoa maoni yao katika warsha hiyo, baadhi ya wajumbe walisema changamoto kubwa imekuwa ni umbali na uchache wa vituo vya kutoa huduma za afya. Aidha, mila na tamaduni za baadhi ya makabila kuhusu mwanamke na mwanaume kuhudhuria vituo vya afya zimechangia changamoto hizi. Wameomba elimu itolewe zaidi kwa jamii ili kufuta dhana potofu zilizopo na kuboresha huduma za afya.

## OFISI YA MKUU WA MKOA WA SINGIDA

*Tunawatakia Kheri ya*

# KRISMASI



2025

# Walimu Kupunguziwa adha ya Usafiri wilayani Iramba



Mkuuu wa Wilaya ya Iramba Mkoani Singida Suleiman Yusuph Mwenda akimkabidhi pikipiki Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Milambo iliyopo Kijiji cha Mingela Kata ya Ntwike, Tarafa ya Shelui Wilayani Iramba, Mwalimu Hussein Kionda,kwa lengo la kuondoa changamoto ya usafiri unaomkabili Mwalimu huyo katika kutimiza majukumu ya kazi yake.

01 November 2024

Mkuuu wa Wilaya ya Iramba Mkoani Singida Suleiman Yusuph Mwenda akimkabidhi pikipiki Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Milambo iliyopo Kijiji cha Mingela Kata ya Ntwike, Tarafa ya Shelui Wilayani Iramba, Mwalimu Hussein Kionda,kwa lengo la kuondoa changamoto ya usafiri unaomkabili Mwalimu huyo katika kutimiza majukumu ya kazi yake.

Mwenda ameyasema hayo Novemba 1,2024 wakati akimkabidhi pikipiki Mwalimu Hussein Kionda nje ya Viwanja vya Ofisi ya Mkuu wa Wilaya na kuhudhuriwa na Kaimu Afisa Elimu idara ya Elimu Awali na Msingi Agnes Peter.

Aidha Mwenda amesema kuwa , kutokana na Changamoto kubwa ambayo ilikuwa inamkabili mtumishi huyo kutoka na ukosefu wa miundo mbinu ya Barabara na hakuna Usafiri wa Aina yoyote Unaoweza kufika Eneo hilo na hakuma huduma muhimu, ilimfanya mtumishi huyo kupata shida ya kufika na kufanya kazi zake ipasavyo.

"Malengo ya Wilaya ya Iramba katika Ufaulu ni kufika Asilimia 100 % na Kwa Sasa tupo kwenye Asilimia 77% hivyo tukio hili litakuwa Endelevu Kwa Shule zote na kuhakikisha kuwa tumeziondoa.Tumekuwa tukitoa Motisha kwa walimu na Wanafunzi wanaofanya vizuri kitaaluma mwaka huu





tulitoa Kompyuta kwa Kila Shule zilizofanya vizuri kitaaluma kwa Kata 20" Amesema DC Mwenda.

Kipekee nimpongeze na Kumshukuru Afisa Elimu idara ya Elimu Awali na Msingi Mwalimu Rose Kibakaya,Amekuwa msikivu na Kila mara tumekuwa tukipanga mikakati ya Kuinua ufaulu kwa kuhakikisha tunatoka Motisha kwa walimu na Wanafunzi wanaofanya vizuri.

"Tunashirikiana na Wanafunzi wa Shule ya Vestfyns Efterskole iliyopo Mji wa Tomerrup

Nchini Denmark wamefanya ziara ya Kutembelea maeneo mbalimbali ya Wilaya ya Iramba kwa lengo la kukuza ushirikiano,Mwaka Jana walikuja Wilayani kwetu kujifunza mambo mbalimbali na Sisi tumepanga mwishoni mwa Mwaka huu tutawapeleka wanafunzi 25 na walimu na Wakuu wa Shule za Sekondari za Lulumba na Tumaini ziara Nchini humo ikiwa ni Mikakati niliyoiweka ya kuhakikisha Kila anayefanya vizuri atakuwa anapata Motisha" Amesema DC Mwenda

# "Toeni Elimu Ya Chanjo Kwa Jamii " DED Matomora



Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Iramba Ndg. Michael Agustino akizungumza na watoa huduma za afya pamoja na wakuu wa vituo vya kutolea huduma za Afya wilayani Iramba Singida.

06 December, 2024

Timu ya Uendeshaji huduma za Afya Wilaya (CHMTs) na Wakuu wa vituo vya kutolea huduma za Afya Wilaya ya Iramba Mkoani Singida wametakiwa kutoa elimu ya umuhimu wa chanjo kwa jamii ili kurahisisha shughuli hiyo ya utoaji chanjo itakavyoanza badaye mwezi huu.

Kauli hiyo imetolewa Ijumaa Disemba 6,2024 na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Iramba Ndugu Michael Agustino Matomora katika kikao cha tathmini ya takwimu za idara ya afya kwa robo ya mwezi julai hadi septemba 2024 na maandalizi ya wiki ya chanjo.

Amesema pamoja na kutoa elimu kwa wananchi wahakikishe wanawatafuta watoto waliohasi chanjo ili wapate huduma hiyo itakayowasaidia kujilinda na maradhi mbalimbali.

"Kwa sasa tuna asilimia 5 ya watoto waliohasi chanjo, tukawatafute na kuwapa chanjo pamoja na kuweka mikakati endelevu ya kuzuia kuhasi tena chanjo hizi." Alisema Matomora.

Aidha, Matomora alielekeza kuboresha viashiria vya afya ya uzazi na mtoto ikiwa ni pamoja na kuweka mkakati wa kuhakikisha wajawazito wanajifungua katika vituo vya afya, mbapo kwa sasa ni asilimia 83 ya wajawazito wanaojifungua katika vituo hivyo ikiwa ni chini ya lengo la asilimia 95.

Pia amesisitiza kuhusu utekelezaji wa sera ya uzazi wa mpango ili kufikia malengo ya Serikali katika sera hiyo.

Akitoa takwimu za chanjo kwa robo ya Julai hadi Septemba Mganga Mkuu Halmashauri ya Wilaya ya Iramba Dkt. Glory Cleophace Andrew alisema bado kuna changamoto ya baadhi ya watoto ambao hawapati chanjo na hivyo kwa sasa imewekwa mikakati ya kuzuia hali hiyo ili kuondoa hatari ya magonjwa ya milipuko.

"Kwa mwaka uliopita kulikuwa na milipuko ya surua, baadhi ya maeneo lakini pia Wilaya ya Iramba ilitugusa kidogo. Pia Kuna magonjwa mengine ambayo kama hatutafanya shughuli hii ya chanjo vizuri milipuko hii inaweza ikatokea" Alisema Dkt. Gloria Cleophace Andrew

Wiki ya chanjo inatarajiwa kuanza Decemba 16, 2024 na itakamilika decemba 20 mwaka huu kwenye vituo vyote 49 vinavyotoa huduma ya chanjo.

# ZIARA: Iramba yanufaika na Ujio wa Idara ya Vitengo

*Mkuu wa Idara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi Halmashauri ya Wilaya ya Iramba Bi. Marietha Kasongo akiongoza mjadala wa Majumuisho ya ziara ya Wakuu wa Idara na vitengo mbalimbali pamoja na Madiwani kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Masasi, tarehe 04/12/2024 katika ukumbi mdogo wa mikutano wa Halmashauri ya Wilaya ya Iramba.*

*Ziara hiyo ya siku mbili ilianza tarehe 03-04/12/2024 katika kata ya Mtoa, kata ya Shelui pamoja na kata ya Ulemo. Na ilianbatana na mafunzo yanayo husu upatikanaji wa mbegu za Alizeti, Elimu ya Ugani, uandaaji wa mashamba, masoko, Viwanda vya kusindika, Wajasiliamali wa Mafuta, Vikundi vya Wajasiliamali wa Bidhaa zinazotokana na zao la Alizeti. Pia ilihusisha kuwatembelea baadhi ya wakulima wa zao hilo katika kata ya Mtoa.*

# "Lazima mji wetu wa Manyoni uwe safi" Mary Kanumba

14 December, 2024

Haya yamesemwa na Mary Kanumba Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni Leo tar 14 Disemba 2024 kwenye kikao cha Wenyeviti wa vitongoji na mabalozi wa Kata ya Manyoni pamoja na wadau wa usafi wa Mazingira.

"Lazima mji wetu wa Manyoni tuhakikishe unakua safi kwa kuzingatia taratibu zote za usafi lakini ikiwa ni pamoja na kuunga mkono mkakati wa taka zetu kuzolewa na kupelekwa sehemu iliyotengwa ila kuepuka magonjwa ya milipuko".

Naye Swed Seifu Mkuu wa kitengo cha Kudhibiti taka na usafi wa Mazingira amesema ni lazima tuhakikishe tunaweka Mazingira katika hali ya usafi kwa kufuata utaratibu wetu wa kutunza taka sehemu nzuri na hatimae taka hizo kupitiwa na magari na kwa ratiba ambayo mtapewa, Jitihada za kutunza Mazingira na kuyaweka safi ni jukumu letu sote Ili kuepuka magonjwa ya milipuko kama kipindupindu.

Kwa upande wa Kampuni ya JAKAIT INTEGRITY SERVICES ambao ndio wamepata zabuni ya kuzoa taka na kuweka mji wa Manyoni safi Ndg Lameck Ladsilaus Afisa Masoko akizungumza kwa niaba ya Mkurugenzi wa Kampuni amesema.

" Sisi ni wazoefu sana kwa Kazi hii tumefanya kwenye miji mingi, tunaahidi kushirikiana nayi vizuri Ili kazi yetu iwe rahisi, Tunatoa kipaumbele kwa vijana wenyeji katika kazi hii ili nao pia wapate ajira na kipato kupitia kazi hii ya uzoaji taka"

Diwani Kata ya Manyoni Mhe. Simon Mapunda amewaomba Wenyeviti wa vitongoji na mabalozi kuwapa ushirikiano wa kutosha wadau hawa waliopata zabuni hii na kuhakikisha wanatoa Elimu na taarifa vizuri kwa wananchi Ili kurahisisha zoezi hili la kuweka mji wa Manyoni safi.

# Kikao cha Kamati ya Lishe chafanyika Manyoni

13 December, 2024

Mhe. Dkt Vincent Mashinji Mkuu wa Wilaya Manyoni leo 13 Disemba, 2024, ameongoza kikao cha Kawaida cha Tathmini ya Utekelezaji wa Mkataba wa Lishe kilichofanyika kwenye Ukumbi wa Mikutano wa Halmashauri ya Manyoni chenye lengo la kupokea na kupitia utekelezaji wa Tathmini ya Hali ya Lishe kwa Ngazi ya Kata kwa robo ya pili (Semptemba - Desemba 2024.)

Akifungua kikao hicho kilichofanyika kwenye ukumbi wa Mikutano wa Halmashauri ya Manyoni, amewataka wajumbe wa kikao hicho kufahamu kuwa lishe ndio msingi wa kila kitu na kwamba kikao hicho ni muhimu katika uboreshaji wa lishe katika jamii na kuwasihi kusimamia afua za lishe kwenye maeneo yao kwa kuzingatia vigezo vya Kitaifa ili kuwa na Jamii yenye afya bora.

Sambamba na hilo, amewasisitiza Wakuu wa Shule za Sekondari na Msingi kuendelea kuhakikisha wanatoa chakula mashuleni ikiwa ni sehemu ya kumuunga mkono Rais wa Jamhuri ya Muungano Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan ambapo suala la lishe shuleni katika uongozi wa Awamu ya Sita ni kipaumbele.

Awali akieleza mafanikio katika utekelezaji wa viashiria vya lishe vinavyopimwa na Mkataba kwa Ngazi ya Wilaya, Mratibu wa Lishe Bw. Sambu Nala amesema viashiria vyote 11 vinavyopimwa katika utoaji wa huduma za lishe vimetekelezwa vizuri kwa kufikia kufikia hali nzuri ya utekelezaji, huku mafanikio yaliyopatikana kwenye utekelezaji kwa ngazi ya Kata ni kuimarika kwa ushirikiano kwa ngazi ya vituo, jamii na viongozi wa ngazi mbalimbali toka Wilaya hadi Mitaa pamoja na lishe kuwa swala mtambuka na kuongelewa katika ngazi mbalimbali za vikao katika jamii hasa kupitia watendaji na watoa huduma ngazi ya jamii.





# Shule ya Msingi Unyamikumbi Yaboreshwa Kupitia BOOST





*Majengo ya madarasa ya Shule ya Unyamikumbi yaliyokamilka baada ya ujenzi kupitia mradi wa BOOST wa mwaka 2023 - 2024. Pamoja na hayo majengo haya yatrahisisha katika huduma ya utoaji wa elimu mkoani Singida.*

11 December, 2024

Shule ya sekondari Kimpungua, iliiyopo kata ya misuna Manispa ya singida ikiwa imekamilika. Shule hii iliyopokea fedha kiasi cha Tshs.184,000,000.00 kwaajili ya ujenzi wa vyumba nane.



# Vikundi 17 kunufaika kwaTsh 278.2 m mikopo ya asilimia 10




*Vikundi vya wanawake, vijana na wenye ulemavu katika picha ya pamoja na Mhe. Ally Mwanga akimwakilisha Mbunge wa jimbo la Singid Magharibi nje ya Ofisi ya Wilaya ya Ikungi mara baada ya zoezi la kupewa mkopo kwa vikundi 17*

14 December, 2024

Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi yakabidhi hundi ya zaidi ya milioni 278.2 kwa vikundi 17 mkopo wa asilimia 10 wa wanawake,vijana na walemavu, hatua Kali kuchukuliwa kwa watakaoenda kinyume na makubaliano yaliyowekwa dhidi ya mkopo huo.

Hayo yamesemwa hii leo tarehe 20 Disemba 2024 katika ukumbi wa Halmashauri na Mhe Ally Mwanga akimuwakilisha Mbunge wa jimbo la Singida manghahari Mhe Elibariki Kingu kuwa kumeibuka tabia ya vikundi kubadili matumizi ya fedha za mikopo na wengine kukimbia na fedha hizo.

"Hatua Kali za kisheria zitachukuliwa kwa wote watakaofanya hivyo" amesema Mwanga.

Mkurugenzi Mtendaji Ndg Justice Kijazi akisoma taarifa amesema kuwa halmashauri ya wilaya ya Ikungi tayari ilikuwa imeshatoa mikopo yenye thamani ya milioni 852.1kwa vikundi 271 vya wanake vijana na watu wenye ulemavu ambapo kati ya fedha hizo vikundi 186 vya wanawake vilipatiwa mikopo yenye thamani ya milioni 476.9, vikundi vya vijana 58 mikopo ya Shilingi 303.2 na vikundi vya watu wenye ulemavu 27 mikopo ya milioni 71.9 na kupekekea jumla ya wanufaika 1870 walipata mikopo hiyo iliyowawezesha kutekeleza miradi mbalimbali ya ujenzi, ufugaji , kilimo biashara ndogondogo na Tehama.

Kijazi ametaja changamoto zilizopo katika utoaji wa mikopo ya asilimia 10 kuwa ni pamoja na baadhi ya vikundi kutorejesha mikopo kwa wakati, vikundi kubadili matumizi ya fedha walizokopeshwa hata kabla ya kutekeleza miradi waliyoombea fedha, mabadiliko ya hali ya hewa kuathiri miradi ya Kilimo,uhaba na bei kubwa kwa baadhi ya malighafi za miradi hivyo kukwamisha uendelevu wa miradi

Kukosekana kwa mtandao wa usajili kwenye baadhi ya maeneo,uhaba wa vitendea kazi kwa wataalam wanaoratibu mikopo hii hususan usafiri, vifaa vya kusajilia vikundi kwa njia ya kielektroniki laptop na vishkwambi na vifaa vya hamasa kama vile vipaza sauti na kutokuwepo kwa mafunzo ya kina kwa vikundi.

"Kwa niaba ya wananchi wa Ikungi naishukuru Serikali ya Awamu ya 6 chini ya Mhe.Rais Daktari Samia Suluhu Hassan kwa kuona umuhimu wa mikopo hii kwa wananchi na kuridhia ianze kutolewa tena baada ya kuboreshwa taratibu wa utoaji na usimamizi wa mikopo hii" amesema Kijazi





# Jeshi la akibaikungi wahitimu mafunzo.

23, November 2024

Askari wa jeshi la akiba 141 wanaume ikiwa ni 121 na wanawake 20 wilaya ya Ikungi wahitimu mafunzo yaliyodumu kwa zaidi ya miezi mitatu katika kata ya Kituntu wilayani hapa.

Akizungumza wakati wa kufunga mafunzo hayo tarehe 23 Novemba, 2024 mkuu wa Wilaya ya Ikungi Mhe Thomas Apson amewapongeza wote walioonyesha nidhamu mpaka kufiki siku ya kuhitimisha mafunzo hayo na kuwaomba waende kuwa mabalozi wazuri ili kudumisha amani katika Wilaya hii.

Hata hivyo amempongeza Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi Ndg. Justice L. Kijazi kwa kuonyesha ushiriki wake katika kila yanapotokea mafunzo ya jeshi la akiba kwa kutatua changamoto mbalimbali akishirikiana na madiwani.

Mkuu wa Wilaya amesema kuwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayoongozwa na Rais Dkt Samia Suluhu Hassan imekuwa ikitoa kipaumbele kwa waliopata mafunzo ya jeshi la akiba Mgambo kujiunga na jeshi la kujenga taifa na kuwapa fursa mbalimbali zinazojitokeza ndani ya Wilaya na hata kwingineko

Kwa upande wake Kaimu mshauri wa Mgambo Wilaya ya Ikungi amesema kuwa kambi hiyo ilipokea jumla ya wanafunzi 192 wanaume 154 na wanawake 38 na kati yao wanafunzi 42 hawakuendelea na mafunzo baada ya kuchaguliwa kujiunga na Jeshi la kujenga taifa kwa kujitolea na wanafunzi tisa hawakumaliza mafunzo kwa sababu za utoro.

"Wanafunzi hao wamesoma masomo mbalimbali na lengo kuu ni kuwajengea uzalendo, kuwajengea ukakamavu, kudumisha nidhamu na kuwaweka tayari kwa lolote litakalotokea" amezungumza mshauri wa Mgambo






# Changamoto Za Kifedha Kutafutiwa Utatuzi Singida



Mkuu wa Mkoa Singida Mhe. Halima Dendego (katikati) kushoto ni katibu tawala wa mkoa wa Singida Dkt. Fatuma Mganga, kulia ni mkuu wa wilya ya Singida Mh. Godwin Gondwe wakiwa katika kikao cha Kujadili Changamoto za Kifedha na Utatuzi wake ndani ya Mkoa wa Singida akiwa pamoja na Viongozi wa BoT (Bank of Tanznaia) na wadau wngine wa kimaendeleo.

02 December 2024

Benki Kuu ya Tanzania (BoT) imesema asilimia 10 tu ya watu wazima mkoani Singida ndio wanaotumia huduma za benki, kiwango ambacho kipo chini ukilinganisha na kiwango cha kitaifa ambacho ni asilimia 22.

Kaimu Meneja Msaidizi sera na chambuzi za huduma za kifedha kutoka BoT, Edmund Mbokosi, alisema hayo leo katika kikao cha kujadili changamoto za kifedha na utatuzi wake mkoa wa Singida, ambacho kimewashirikisha Wakuu wa Wilaya, Wakurugenzi wa Halmashauri, na mameneja wa benki zinazotoa huduma za kifedha mkoani hapa.

Amesema katika huduma za kifedha, mkoa wa Singida wanatumia asilimia 50 wakati wastani wa kitaifa ni asilimia 72. Bima ni asilimia 5, huduma za vyama vya kuweka na kukopa (SACCOS) Singida ni asilimia 7, wakati lengo la kitaifa ni asilimia 12.

Mbokosi amesema kutokana na changamoto hiyo BoT imeamua kutoa elimu ili kuangalia namna ya kuweza kupandisha kiwango cha matumizi ya huduma za kifedha katika mkoa wa Singida kwa lengo la kuufanya mkoa kupanda kiuchumi na kuondoka katika nafasi ya tatu kutoka mwisho.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Singida, Halima Dendego, amesema mkoa utajitathmini kwenye sensa kwa kupitia kwenye maeneo mbalimbali kama kwa wanafunzi mashuleni na vyuoni vilivyopo mkoani hapa ili kupandisha kiwango cha huduma za benki.

"Tuna vyuo vingine na taasisi nyingine karibu kila mtu anatakiwa kulipwa pesa kupitia benki na hivi sasa kuna huduma mpya mfano ya mfumo wa stakabadhi ghalani kwa hiyo nina imani kiwango cha asilimia 72 cha huduma za kifedha tutakifikia," alisema.

Awali, Mchambuzi Maswala ya Fedha kutoka BoT, Michael Mwaituka, alisema BoT imejipanga kuwasaidia wajasiriamali nchini kupitia Mfuko wa Udhamini wa Mikopo kwa ajili ya Mauzo Nje ya Nchi (ECGS) pamoja na Mfuko wa Udhamini wa Mikopo kwa Wajasiriamali Wadogo na wa Kati (SME-CGS).





Amesema lengo la kuwezesha sekta binafsi wenye miradi mizuri kuweza kupata mtaji kutoka kwenye mabenki na taasisi za fedha zilizosajiliwa chini ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha 2006, pale wanapokuwa na upungufu wa dhamana.

Mwaituka amesema kuwa BoT wanashughulikia Mfuko wa Udhamini wa Mikopo kwa niaba ya serikali ili kuwasaidia Watanzania kupata mitaji kuongezea uzalishaji, ajira, fedha za kigeni na pato la taifa kwa ujumla.

Amesema kuwa Mfuko wa Udhamini wa Mikopo kwa Wajasiriamali Wadogo na wa Kati una lengo la kuwawezesha wajasiriamali wadogo na wa kati wenye miradi mizuri lakini wanaupungufu wa dhamana, kuweza kupata mitaji kutoka kwenye mabenki na taasisi za fedha zinazohusika na Benki Kuu.

**KUMBUKA**

***"Mali Bila Daftari Hupotea Bure"***

# Wakulima Changamkieni Mbegu na Mbolea za Ruzuku



*Mkuu wa Wilaya ya Makalama Mhe. Moses Machali akiwa kwenye mkutano na wakulima wilayani kwake huku akitoa rai kwa wakulima kujisajili katika mfumo ili waweze kupata mbegu na mbolea za ruzuku wilayani hapo.*

16 December 2024

Mkuu wa Wilaya ya Mkalama, Mhe. Moses Machali, ametoa rai kwa wakulima wilayani Mkalama kujisajili katika mfumo ili waweze kupata mbegu na mbolea za ruzuku.

Ameitoa kauli hiyo leo, Desemba 16, 2024, katika kijiji cha Ilunda, Kata ya Ilunda, wakati wa hafla ya kumkabidhi mshindi wa tuzo ya Mkulima Bora Kitaifa wa Maonesho ya Nane Nane 2024 yaliyofanyika katika viwanja vya Nzunguni, Jijini Dodoma.

"Serikali ilianza na mbolea na sasa imeanza kutoa ruzuku kwenye mbegu za mahindi na alizeti. Wito wangu ni kununua na kuhakikisha mnakwenda kujisali ili muweze kupata mbegu kwa bei nafuu," alisema Mhe. Machali.

Akizungumzia suala la utunzaji wa mazingira, Mhe. Machali aliwataka wakazi wa kijiji cha Ilunda kupanda miti kwa wingi ili kupambana na uharibifu wa mazingira.

"Tukiwa na miti mingi, tutapata mvua za kutosha na tutakuwa tumetunza mazingira," alisema Machali.

Aidha, aliwakumbusha wakazi wa Ilunda na Mkalama kwa ujumla kujiepusha na vitendo vya uvunjifu wa amani, kufanya kazi kwa bidii pamoja na kujilinda dhidi ya ugonjwa wa UKIMWI.

Akizungumza wakati wa hafla hiyo, Suzana Mwakiro alisema tuzo iliyotolewa ni chachu kwa kila mmoja kupambana na kuhakikisha kilimo kinakua sehemu ya kumuinua kila mmoja katika nyanja ya kiuchumi na kijamii, huku pia kikiwa chanzo cha kuwapatia wananchi chakula cha kutosha.

"Kilimo ni uti wa mgongo wa Watanzania. Hivyo, ni jukumu letu kuhakikisha tunafaidi matunda yake kwa kuhakikisha tunazitumia vyema fursa za mbegu na mbolea za ruzuku tunazopewa na serikali kwa mavuno mengi na bora," alisema Suzana.



## Mkoa wa Singida wajiandaa Kukabiliana na Ugonjwa wa Kipindupindu

22 December 2024

Katibu Tawala wa Mkoa wa Singida ameagiza uwajibikaji kwa timu ya uratibu wa afya ya mkoa kuhakikisha wanajituma na kufanya kazi kwa weledi ili kuepusha mlipuko wa ugonjwa wa kipindupindu katika Mkoa wa Singida.

Ameyasema hayo katika kikao kazi cha kujadili namna ya kukabiliana na ugonjwa wa kipindupindu kilichofanyika leo, Novemba 22, 2024, katika ukumbi wa Mkuu wa Mkoa wa Singida.

Kikao hicho kiliratibiwa na Mganga Mkuu wa Mkoa wa Singida, Daktari Victorina Ludovick, na kilihudhuriwa na wawakilishi wa timu ya afya ya mkoa, maafisa kutoka halmashauri mbalimbali, pamoja na viongozi wa jamii.

Katika kikao hicho, Katibu Tawala alisisitiza umuhimu wa kuchukua hatua za haraka za kinga, kuimarisha huduma za usafi wa mazingira, pamoja na kutoa elimu kwa jamii kuhusu dalili za ugonjwa wa kipindupindu na hatua za kuchukua iwapo mtu anadhani ameathirika.

Daktari Victorina Ludovick alisema kuwa ugonjwa wa kipindupindu ni tishio kwa afya ya jamii hasa wakati wa msimu wa mvua, hivyo ni muhimu kwa kila mdau kushiriki katika juhudi za kudhibiti ugonjwa huo kwa kuhakikisha upatikanaji wa maji safi na salama, pamoja na matumizi ya vyoo bora.

# Wajasiriamali Wadogo Wadogo Kunufaika Na Vitambulisho Vya Kidijitali



*Mkuu wa wilaya ya Singida Godwin Gondwe akiwa katika zoezi la uzinduzi wa Ugawaji wa Vitambulisho vya kidijitali kwa Wajasiriamali wadogowadogo mkoani Singida akimwakilisha mku wa Mkoa.*

05 December 2024

Mkuu wa Wilaya ya Singida, Godwin Gondwe, leo Disemba 05, 2024, amemuwakilisha Mkuu wa Mkoa wa Singida, Halima Dendego, katika uzinduzi wa zoezi la ugawaji wa vitambulisho vya kidijitali kwa wajasiriamali wadogo wadogo mkoani Singida.

Uzinduzi huo umefanyika katika Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Singida.

Uzinduzi huo umehudhuriwa na viongozi na wawakilishi mbalimbali, akiwepo Katibu Tawala Msaidizi sehemu ya viwanda na biashara, Maafisa maendeleo ya jamii kutoka ngazi za mkoa na halmashauri ambao ni waratibu wa dawati la wafanyabiashara ndogo ndogo, viongozi wa wafanyabiashara ndogo ndogo (wajasiriamali), na wawakilishi kadhaa wa wafanyabiashara ndogo ndogo.

Akizungumza wakati wa hafla hiyo, Mkuu wa Wilaya amesema ni wakati sasa wa wajasiriamali kwenda kunufaika na fursa mbalimbali kutokana na kupata vitambulisho hivyo huku akitoa agizo kwa waratibu wa zoezi hilo wilaya zote kuongeza kasi ya kuandikisha wajasiriamali hao ili wengi waweze kunufaika.

"Shughuli ya uzinduzi na ugawaji wa vitambulisho vya kidijitali kwa ajili ya Wafanyabiashara ndogo ndogo katika Mkoa wa Singida umetokana na changamoto ya muda mrefu ya kutaka kuwatambua wafanyabiashara ndogo ndogo nchini kwa idadi yao na umuhimu wa kuweka utaratibu mzuri wa kuwaratibu ili waweze kufanya shughuli zao za kiuchumi na kijamii kwa lengo la kuwainua wafanyabiashara hao kiuchumi na kijamii pamoja na utayari wa kuhakikisha kuwa changamoto zao zinapatiwa ufumbuzi na wataalam kwa wakati," alisema DC Gondwe.

Awali, Katibu Tawala Msaidizi sehemu ya viwanda na biashara, Bi. Donatila Vedasto, ameainisha makundi ya Wafanyabiashara ndogo ndogo:

"Wafanyabiashara ndogo ndogo nchini tunazingatia biashara zote halali zinazofanywa na wafanyabiashara hao ambazo zinatambuliwa na mamlaka. Aidha, wafanyabiashara ndogo ndogo wanajumuisha machinga, mama na baba lishe, madereva wa bodaboda na bajaji, wasusi, vinyozi, wakulima wa bustani ndogo ndogo na wauzaji wa vyakula kama vile matunda na mboga mboga. Kwa ujumla sekta hii inachangia kwa kiwango kikubwa kutoa ajira kwa vijana wanaohitimu katika ngazi mbalimbali za elimu na taaluma hapa nchini," alisema Bi. Donatila.

Wema Yona, mfanyabiashara ambaye amepata kitambulisho siku ya leo, amesema





anategemea kupata fursa nyingi zaidi kupitia vitambulisho hivyo vya wafanyabiashara ndogo ndogo ikiwemo fursa za kupata mikopo ambazo walikuwa hawazipati, akisema kuwa sasa watafanya kazi kwa kujiamini zaidi huku akitoa wito kwa wajasiriamali wote kupata vitambulisho hivyo ili kuwa karibu na fursa.

Pia, ameomba ushirikiano wa kutosha kutoka kwa viongozi uendelee ili kuweza kuzitatua changamoto zitakazojitokeza kwa lengo la kukuza uchumi wa wajasiriamali mmoja mmoja na Singida kwa ujumla kwa kuongeza mapato kutokana na kulipa kodi.

Mpaka sasa, takribani wajasiriamali 894 wameshasajiliwa na kupata vitambulisho hivyo mkoani Singida.



# Manyoni na Itigi Kunufaika na Utunzaji wa Misitu ya Asili




*Mkuu Mkoa wa Singida Mhe. Halima Dendego akiwa katika hafla ya upandaji miti wakati wa kusherehekea miaka 63 ya Uhuru wa Tanznaia*

09 December 2024

Wilaya za Manyoni na Ikungi katika Mkoa wa Singida zinatarajiwa kupokea mabilioni ya fedha kutokana na utunzaji wa misitu ya asili, vichaka vya Itigi (Itigi Thickets), ambavyo ni adimu duniani na vinapatikana katika Bara la Afrika, hasa Tanzania na Zambia pekee.

Mkuu wa Mkoa wa Singida, Mheshimiwa Halima Dendego, alisema hayo wakati wa maadhimisho ya miaka 63 ya Uhuru wa Tanzania Bara yaliyoadhimishwa kwa viongozi wa chama, serikali, na wananchi kwa kupanda miti 501 katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Singida.

Kabla ya zoezi la kupanda miti hospitalini hapo, Dendego aliongoza viongozi wa chama, serikali, na wananchi kutembelea katika wodi za wagonjwa kuwapa faraja na kuwapa zawadi mbalimbali.

Mheshimiwa Dendego alisema mkakati mwingine uliopo ni kutengeneza mpango wa matumizi ya ardhi, kuendelea kuhifadhi misitu ya asili kwani misitu ni fedha kutokana na biashara ya hewa ya ukaa yenye faida nyingi na Mkoa wa Singida utakuwa miongoni mwa wanufaika wa fedha hizo.

"Wilaya yetu ya Manyoni na Ikungi ipo mbioni itaanza kupokea mabilioni ya fedha muda mchache ujao. Niwapongeze wakuu wa wilaya kwa kupambana maana wananchi wetu wakiona kitu ndo wataamini, miti yetu ni dhahabu ya kijani," alisema Dendego.

Dendego alisisitiza kuwa mkoa utaendelea na zoezi la kuhamasisha upandaji miti, ambapo zoezi rasmi litafanyika Januari 2025 na kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia ili kunusuru misitu.

"Vipo vijimitu vya asili au vichaka vya Itigi, Manyoni na Ikungi. Tunaviona kama ni maeneo hatarishi lakini kumbe ni mazalia ya tembo, yaani tembo anapotaka kuzaa ndo anakwenda kwenye vile vichaka," alisema Dendego.

Awali, Afisa Maliasili wa Mkoa wa Singida, Charles Kidua, alisema miti 13,399,031 ambayo ni kati ya miche 33,253,602 iliyopandwa katika Mkoa wa Singida katika kipindi cha kuanzia 2019 hadi 2024 imekufa kutokana na sababu mbalimbali ikiwa ni pamoja na utunzaji hafifu.

"Katika uhifadhi wa misitu na mazingira, mkoa umepanda jumla ya miche ya miti 33,253,602 sawa na asilimia 63 ya lengo kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita na miti iliyopo ni 19,854,571 sawa na asilimia 59.7 ya miti iliyopandwa," alisema Kidua.

Kidua alitaja sababu za miti mingi inayopandwa kufa ni kutokana na uharibifu unaofanywa na mifugo, utunzaji hafifu, mchwa kuharibu miche, kuwepo kwa vipindi virefu vya jua, na uelewa mdogo wa wananchi juu



ya matumizi ya nishati safi ya kupikia.

Alisema katika kipindi hiki cha mvua, miti 1,768,192 imepandwa katika maeneo mbalimbali ya Mkoa wa Singida ambapo mkoa utaendelea na zoezi la upandaji miti ipatayo 5,395,909 katika vyanzo vya maji, taasisi za serikali, watu binafsi, na taasisi za kidini hadi mwisho wa msimu huu wa mvua.

Kidua alieleza kuwa mkoa umejiwekea dira na mwelekeo wa kuongeza utekelezaji wa upandaji miti kutoka asilimia 63 ya sasa mpaka asilimia 90 ifikapo 2030 na kuongeza idadi ya misitu ya hifadhi kufikia hekta 100,000 ifikapo 2030.



# Kamati ya usalama wilayani Manyoni yafanya ziara kukagua Utekelezaji miradi



*Kamati ya Usalama ikiongozwa na mkuu wa Wilaya ya Manyoni Mhe. Dr. Vincent Mashinji, wakiwa katika ukaguzi wa maendeleo ya mradi wa ujenzi wa shule na miradi mingine Mkoani Singida*

11 December 2024

**M**wenyekiti wa Kamati ya Usalama ambaye pia ni Mkuu wa Wilaya ya Manyoni, Mhe. Dkt. Vincent Mashinji, akiwa ameambatana na kamati ya usalama, wamefanya ziara ya kukagua maendeleo ya utekelezaji wa miradi.

Ziara hiyo imefanyika leo, Disemba 11, 2024, ambapo miradi mbalimbali imekaguliwa, ikiwemo mradi wa ujenzi wa Shule ya Ufundi ya Sekondari Amali (Kintinku - Lusilile). Dkt. Mashinji aliwataka wasimamizi wa mradi huo kuhakikisha unakamilika kwa wakati.

Kamati hiyo imekagua pia ujenzi wa shule mpya ya msingi (Tambukareli), ujenzi wa miundombinu ya kidato cha tano Shule ya Sekondari Manyoni pamoja na Mradi wa Shule mpya ya sekondari Matori (Manyoni).

Dkt. Mashinji ameagiza kuwa miradi hiyo ikamilike ndani ya wakati ili ifikapo Januari 15, 2025, shule zinapofunguliwa wanafunzi waweze kutumia madarasa hayo. Ziara hiyo itaendelea katika jimbo la Manyoni Mashariki.





# Watumishi na Viongozi Mkoani Singida Wapewa Mafunzo Kuinua Utendaji Kazi



*Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi Ndg. Justice L. Kijazi akifungua mafunzo ya Kuboresha Utendaji kazi wa wafanyakazi wa serikali kuanzia ngazi ya vijiji, mtaa, na vitongoji.*

18 December 2024

**K**atika kuhakikisha viongozi wanafanya kazi zao kwa uadilifu na utawala bora, madiwani, wakuu wa divisheni na vitengo, wenyeviti wa vijiji, mitaa, na vitongoji katika Wilaya ya Ikungi na Halmashauri ya Singida wamepatiwa mafunzo kwa ajili ya kuboresha utendaji wao wa kazi ili kuwa daraja zuri katika kuwaunganisha wananchi na serikali.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi, Ndg. Justice L. Kijazi, alifungua mafunzo hayo ambayo yalianza tarehe 16 Disemba 2024 na yanatarajiwa kuendelea hadi tarehe 20 Disemba 2024. Mafunzo hayo yanahusisha mada mbalimbali, zikiwemo za uboreshaji wa utendaji kazi wa viongozi wa umma.

Mkurugenzi Kijazi alisema mafunzo hayo pia yanahusisha ujuzi wa ujazaji wa tamko la maadili kwa viongozi kufuatia matakwa mapya ya Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma kuhusu ujazaji wa tamko la rasilimali na madeni kwa njia ya mfumo wa kielektroniki kwa mujibu wa sheria.

"Tumealika viongozi kutoka taasisi mbalimbali ili kutoa mada kuhusu uboreshaji wa utendaji kazi wetu. Hivyo, tutakuwa na mada kutoka taasisi ya kuzuia na kupambana na rushwa (TAKUKURU), tamko la rasilimali na madeni, na masuala ya serikali za mitaa," alisema Mkurugenzi Kijazi.

Mkurugenzi huyo alisisitiza kuwa mwisho wa kujaza tamko la maadili ni tarehe 31 Disemba 2024.

Kwa upande wao, baadhi ya wajumbe wa mafunzo hayo walitoa shukrani kwa Halmashauri kwa kuandaa mafunzo hayo, wakisema kuwa yataongeza tija katika utendaji kazi wao na kuimarisha mahusiano kati ya serikali na wananchi.

Lengo kuu la mafunzo hayo ya siku tano ni kuwawezesha viongozi hao kujifunza masuala ya utawala bora kwa maslahi mapana ya wananchi wa wilaya ya Ikungi na Mkoa wa Singida kwa ujumla.

Kwa upande mwingine, wenyeviti wa vitongoji na vijiji kutoka katika Halmashauri ya Singida walipatiwa mafunzo ya uongozi kwa lengo la kuwajengea uwezo wa uongozi ili kuleta maendeleo kwa wananchi na kusaidia serikali. Mafunzo hayo yalifanyika kwa siku mbili, tarehe 18 na 19 Disemba 2024, katika ukumbi wa Shule ya Sekondari ya Ilongero.

Mafunzo hayo, yanayoratibiwa na Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI), yaliandaliwa na uongozi wa Halmashauri na kutolewa na wawezeshaji kutoka Chuo cha Serikali za Mitaa cha Hombolo.

Mgeni rasmi katika hafla hiyo, Kaimu Katibu Tawala wa Mkoa wa Singida, Bw. Shabani Mongomongo, aliwapongeza wenyeviti wa vitongoji na vijiji kwa kuchaguliwa kuwa viongozi wa wananchi, akiwasihi kusimamia misingi ya uongozi pasipo kuingilia kati utendaji kazi. Sambamba na hilo, alitoa pongezi kwa Chuo cha Hombolo kwa kukubali kutoa mafunzo hayo.

Jumla ya wenyeviti wa vijiji 84 na wenyeviti wa vitongoji 435 walitarajiwa kupatiwa mafunzo hayo kwa siku mbili.ttt





# Mkuu wa Sehemu ya Viwanda biashara na uwekezaji afanya ziara katika halmashauri 5 Mkoani Singida




*Mkuu wa Sehemu ya viwanda biashara na uwekezaji Bi.Donatila D. Vedasto akiwa katika picha wakati wa Ziara kwa kushirikiana na viongozi wa halmashauri ya kijiji cha Mtinko*

Mkuu wa Sehemu ya viwanda biashara na uwekezaji Mkoani Singida, Bi.Donatila D. Vedasto kwa kushirikiana na watumishi wa sehemu hiyo, alifanya ziara katika halmashauri 5 Mkoani Singidaambazo ni manispaa ya Singida,Singida DC, Ikungi, Mkalama na Iramba ambapo alifanya vikao na Maafisa biashara katika halmsahauri hizo na kuweka mikakati mbalimbali ili kuwezesha uchumi wa mkoa wa Singida kukua.

Baadhi ya Mikakati iliyofikiwa ni pamoja na kutoa Elimu kwa wafanyabiashara na kuwapa mbinu za kukuza biashara zao kuwa za kati hadi kubwa,kufanya vikao vya mabaraza angalau mara mbili kwa mwaka kwa mujibu wa mwongozo wa mabaraza ya biashara.

Kufuatilia kwa karibu Vikundi vinavyopewa mkopo ya 10% na kutoa Elimu kwa miradi iliyoibuliwa na vikundi hivyo ili kuhakikisha inafanya kazi, Pia kuhakikisha vinakua na kuwa vikundi vya wafanyabiashara wakubwa.

Kutenga maeneo ya uwekezaji na kutatangaza fursa za uwekezaji zilizopo halmshauri zote za mkoa kupitia njia mbalimbali ili kuvutia wawekezaji.

.kuhakikisha kila halmashauri inaweka katika miradi mbali mbali ili kukuza uchumi wa halmashauri na mkoa kwa ujumla na kuongeza mapato.

Kutambua na kusajili viwanda vidogo vidogo vilivyopo kila eneo na kuhamasisha uanzishaji wa viwanda vingine ikiwa ni pamoja kuvikukuza viwanda vidogo kuwa vya kati hadi vikubwa.

Kuhakikisha wafanyabiashara wanafanya biashara kwa kufuata sheria kanuni na taratibu za kufanya biashara kwa kuwa na vibali vya biashara na kuwawezesha wafanyabiashara wadogo kusajili biashara kuwa na nembo za biashara zao ili waweze kukuza biashara kwa kuongeza masoko.

Kuwaunganisha wafanyabiashara na taasisi za kifedha ili waweze kupata mikopo na kuongeza mitaji yao.

Maafisa biashara katika mkoa wa Singida kufanya kazi kwa mujibu wa sheria na kuhakikisha wanatimiza majukumu yao kwa ufanisi na Kwa wakati.

Aidha,Viwanda mbalimbali vilitembelewa ikiwemo kiwanda cha kijiji cha nyuki,Singida Fresh Oil Mill, Jengo la kongano, Viwanda vya kusaga unga, Kiwanda cha pamba na Mashine za kusaga mahindi.

Wakizungumza na wawekezaji juu ya suala la upungufu wa malighafi za kutosha,Wawekezaji walipewa Elimu na kushauriwa kuwekeza pia katika kilimo cha umwagiliaji kwa kuanzisha mashamba yao wenyewe ili kupunguza au kumaliza kabisa tatizo hilo

Kadhalika, Waliwashukuru wawekezaji wa viwanda hivyo kwa ushirikinao wanaotoa kwa serikali kwa kutoa huduma katika jamii zinazowazunguka na kuwezesha upatikanaji wa maji kwa kuchimba visima,kujenga madarasa, kujenga wodi za kina mama, kujenga mabweni ya watoto na mengineyo

Serikali itaendelea kuwezesha mazingira mazuri kwa wawekezaji wote walipo katika mkoa Singida na kushughulikia changamoto zinazowakabili wawekeza hao.

Hata hivyo w alichukua Fursa hiyo kuwakaribisha wawekezaji kutoka ndani na nje ya mkoa wa Singida na nje ya nchi kuja kuwekeza katika mkoa wa Singida ambao una fursa nyingi sana za kiuchumi.



## MATUKIO KWA NJIA YA PICHA



*Mkuu wa mkoa wa Singida Mhe. Halima Dendego tarehe 26/11/2024 alipozunguza na kusikiliza kero za wananchi. Pia alitoa elimu kuhusu uchaguzi wa Serikali za mitaa na maandalizi yz msimu mpya wa kilimo.*









## MATUKIO KWA NJIA YA PICHA
















# OFISI YA MKUU WA MKOA WA SINGIDA

*Tunakutakia Kheri ya*

# MWAKA MPYA

# 2025

JARIDA LA
SINGIDA RS
TOLEO LA KILA MWEZI KWA MWAKA

# LIMEANDALIWA NA:

## Ofisi ya Mkuu wa Mkoa

Kitengo cha Mawasiliano serikalini
S.L.P. 05 SIngida

Kwa maoni na Ushauri wasiliana nasi kupitia
Simu: 026 250 2089/2249
Fax: 026 250 2078
E-mail: ras@singida.go.tz | info@singida.go.tz

Endelea kutufuatilia kwenye kurasa zetu.

Jarida hili hutolewa na kuchapishwa kila Mwezi